



Kura za maoni zamshusha Trump, Harris ang'ara Uk. 16

Kumekucha Ngorongoro



Kaka kama unavyojua rais akishaa-giza kitu, huna muda wa kupoteza na tayari timu ya watalaam wetu imetembelea kata zote 11 zinazounda Tarafa ya Ngorongoro ili kuanza utekelezaji wa agizo la Rais Samia...”



Habari Uk. 6&7

Soma Ndani

**Onyo:
Hakuna
mafanikio
kupitia
miujiza ya
dini**

KUNDI la Watanza-nia ambao wana-amini kuwa matati-zo yao ya kiuchumi, kifamilia, ndoa na...

Soma zaidi Uk. 26

**Slaa: Samia
alidharau
ushauri
wangu
kuhusu
'ugaidi'
wa Mbowe**

Habari Uk. 14

Wanajeshi wa JWTZ wakiwa kwenye gwaride maalum wakati wa kilele cha maadhimisho ya kutimiza miaka 60 kwa jeshi hilo katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam jana. (Picha na Ikulu)

Miaka 60 ya JWTZ



**DC atumbuliwa
kwa kutangaza
serikali kusaidia
ushindi wa
madiwani CCM**

Habari Uk. 23

**Dkt. Ndugulile
aonya, aeleza
maono WHO**

MBUNGE wa Kigamboni, Dar es Salaam, Dkt. Faustine Ndugulile, ambaye hivi karibuni alichaguliwa kuwa Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Kanda...

Habari Uk. 4



Tahariri/Katuni

Matapeli wanaotumia dini wafungiwe

NDANI ya kurasa za gazeti hili kuna habari inayotoa onyo kwa Watanzania kujiepusha na aina mpya ya utapeli unaofanywa na baadhi ya wale wanaojiita mitume, manabii, maaskofu na hata makuhani – kwa jina la dini.

Hawa ni watu hatari, ambao wameamua kutumia Jina la Mungu kuendelea kuwaibia watu wenye umasikini zaidi; wa mawazo na hata hali, kwa kuwa tu wamejazwa imani.

Pamoja na kwamba watu hao, wapo kisheria baada ya kusajili makanisa yao na kuruhusiwa kuendesha shughuli zao na serikali, lakini kwa uhakika kabisa, wanatumia mwanya huo kutapeli na kuwafukarisha watu wengi zaidi.

Sisi Pambazuko tunao ushahidi wa kutosha tani 1,000 na zaidi, wa kuwepo kundi kubwa zaidi la familia, hasa zinazoongozwa na wanawake, kufilisika kwa kuwa tu zimekumbatia “maagizo ya kuhani, nabii au mtume fulani.”

Maagizo hayo, mara nyingi hutolewa na viongozi wa makundi hayo ya dini kwa kuwajaza imani kwamba waumini wao wanapochanga zaidi fedha kanisani, ndivyo wanaweza kubarikiwa kwa kupokea miujiza.

Wanaokwenda kusali kwa manabii hao, hufa-


nya hivyo kwa malengo maalum; wapo wanaokwenda huko kwa lengo la kupata utajiri, kuimarisha ndoa, kupanda cheo kazini au hata kuvuta wateja wengi zaidi kwenye biashara zao.

Wakifika huko, manabii, mitume au makuhani hao hutumia mwanya wa waumini wao kutokuwa na uelewa wa ndani wa kile wanachokifanya viongozi hao, kuwarubuni na kuwafukarisha zaidi, kwa kuwaibia – kwa mbinu za imani, hata kile kidogo walichonacho kwa manufaa binafsi.

Ndiyo maana hao wanaojifanya kuwa watumishi wa Mungu, kwetu sisi wengi tunawaona ni matapeli tu na wameachwa tu na mifumo yetu kuleta ufukara zaidi kwa Watanzania.

Tunaungana na wanazuoni wa saikolojia wanaoeleza hali hiyo ya kuwepo kwa “mafuriko ya watu” kwa manabii, makuhani na mitume hao, kuwa inasababishwa na msongo wa mawazo na kutindiwa uwezo wa kufikiri sawasawa.

Ni kutokana na madhila mengi yanayopatika na kutoka kwa watu hao wa mungu - wanaomjua wao, serikali iamue kufanya ukaguzi wa makaniha hayo na kubaini yapi yanafukarisha Watanzania ili kuchukua hatua ya kuyafunga mara moja, kabla mabaya makubwa hayajatokea.



Kila la heri Machumu...



Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Mwananchi Communications, Bakari Machumu (kushoto) akiteta jambo na mwandishi mwandamizi, Elias Msuya wakati wa sherehe ya kumuaga mkurugenzi huyo juzi (Picha na Mwananchi)

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: info@pambazuko.or.tz** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Unaweza kusoma gazeti hili kupitia tovuti ya **www.rifaly.com**

TIMU YA PAMBAZUKO

Mhariri Mkuu	:	Simon MKINA	(simon@pambazuko.or.tz)
Mhariri Mtendaji	:	Peter NYANJE	0784 211 716
Mhariri wa Habari	:	Maregesi PAUL	0689 732 325
Mwandishi Mkuu	:	Elizabeth HOMBO	0712 792 216
Mkuu wa DTP	:	Yassin LUPATU	0782 009 971
Mkuu wa Utawala	:	Tryruckia MFINANGA	0744 768 263

Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A - nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz



Dkt. Ndugulile aonya, aeleza maono WHO



Dkt. Faustine Ndugulile

Na Elizabeth HOMBO

MBUNGE wa Kigamboni, Dar es Salaam, Dkt. Faustine Ndugulile, ambaye hivi karibuni alichaguliwa kuwa Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Kanda ya Afrika, amewatahadharisha watu wanaolinyemelea jimbo hilo hivi sasa akisisitiza kuwa yeye bado ni mwakilishi.

Akizungumza mara baada ya kutua Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Dkt. Ndugulile alisema kuwa ataendelea kushikilia wadhifa huo wa Ubunge hadi mwakani.

Dkt. Ndugulile aliwaambia waandishi wa habari uwanjani hapo kuwa atanza kutekeleza majukumu yake kuanzia Februari mwakani – 2025, baada ya kuthibitishwa na vikao vya juu vya WHO.

“Utaratibu wa taasisi za kimataifa unachaguliwa kwanza na baadaye inafanyika michakato ya kuanzishwa, kwa hiyo kikao cha kunithibitisha kitafanyika Februari mwakani huko Geneva, Uswisi,” alisema.

Alisisitiza kuwa kwa sasa ataendelea na majukumu yake ya ubunge kama kawaida hadi Februari mwakani atakapothibitishwa, ndipo atajiuzulu nafasi hiyo ya uwakilishi wa wananchi wa Kigamboni.

“Maswali mengi yamekuwa yanaulizwa ooh sasa jimbo linakuwa wazi, naomba kuwaambia kuwa bado tutaendelea na majukumu yetu mengine ya kawaida hadi hapo Februari mwakani kwa sababu mimi bado siyo mwajiriwa wala mtumishi wa WHO hadi nitakapothibitishwa halafu jimbo litakuwa wazi,” alisema.

Kuhusu atakayofanya kupitia nafasi hiyo, alisema atakwenda kuleta mabadiliko katika mfumo wa uendeshaji wa huduma za afya katika Afrika.

“Hatua tuliyofikia Afrika na Malengo Endelevu ya Dunia, yaani SDGs, inaonyesha kuwa bado tuko nyuma kidogo, nakwenda kuongeza nguvu mpya ili hizi nchi ziweze kupiga hatua nzuri zaidi katika kuhakikisha kwamba tunafikia yale malengo...”

“Asilimia 70 ya vifo vya kinamama viko katika bara letu, asilimia zaidi ya 56 vifo vya watoto duniani viko katika bara letu, ukiangalia hali ya udumavu asilimia 30 uko Afrika...”

“Sasa kwa uzoefu wangu kama mtaalam ambaye nimefanya kazi katika sekta ya afya ndani na nje ya nchi, lakini na uzoefu wangu nikiwa waziri na mbunge, nitakwenda kuweka muunganiko mzuri katika sekta ya afya,” alisema Dkt. Ndugulile.

Dkt. Ndugulile anakuwa Mtanzania wa kwanza kuchaguliwa kushika nafasi hiyo na ataitumikia kwa kipindi cha miaka mitano.

Dkt. Ndugulile alichaguliwa katika mkutano wa WHO Kanda ya Afrika uliofanyika wiki iliyopita huko Brazaville, Jamhuri ya Congo.

“Zaidi nawaahidi utumishi uliotukuka. Nakuwa mtu wa kwanza kwa Afrika Mashariki na Tanzania kushika nafasi hii. Nitashirikiana na Serikali ya Tanzania katika kuboresha mambo mbalimbali ya sekta ya afya na kuwapa ushauri katika mambo ya afya,” alisema Dkt. Ndugulile katika salamu zake za shukran mara baada ya kuchaguliwa.

Mbunge huyo wa Kigamboni kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) anatoa ahadi hiyo kuhusu chanjo wakati Afrika ikikabiliwa na mahitaji makubwa ya chanjo dhidi ya homa ya nyani yaani M-pox.

Akizungumzia kuchaguliwa kwa naibu waziri huyo wa Afya wa zamani, aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Makazi Duniani (UN-Habitat), Profesa Anna Tibaijuka, amemtaka ‘asilale’ kwani Afrika ina matatizo mengi katika sekta ya afya.

Anayetoa siri za ndani CCM akaliwa kooni

Na Igo Al

TANGU jana, Jumapili ya Septemba Mosi, 2024, raia wa Tanzania anayejitambulisha kuwa kada kindakindaki wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mzee Tai ameonekana kupandwa hasira kali.

Hasira zake zinaufikia umma kwa kuwa tangu usiku wa jana, Mzee Tai alionekana akizunguka huku na kule, nje ya ofisi za gazeti la Pambazuko, Mtaa wa Mkapani A, Sayansi, eneo la Kijitonyama, Dar es Salaam, kwa nia ya kutaka kuzungumza na mwandishi wa habari.

Akiwa nje ya ofisi hiyo, majira ya saa 2:30 usiku, alikutana na mwandishi na kuomba akaandike namna alivyojawa hasira kali kwa kuwa eti “kuna mtu anatangaza siri za chama chake.”

Mzee Tai, ambaye alikataa kupanda ngazi kwenda ofisi za gazeti hilo, aliomba aletewe kiti akiwa chini, kwani hawezi kupanda ghorofani kwa hofu ya kutibua zaidi ‘presha’ yake.

“Nimesema lete kiti hapa chini, hatuwezi kuwa na watu wanatoa siri za ndani wanaweka hadharani, yaani watu tumekaa tukatengeneza mipango na mbinu zetu, tukalishana yamini...”

“Kwamba hakuna siri kufikia magazeti, wala kwenye mitandao ya kijamii, sasa nashangaa naona mtu anazomoka, anaweka kila kitu kwenye mitandao, sijui amekula nini huyu, au Chadema wamemroga?”

“Inawezekanaje sisi viongozi wote wa Longido, kwa maelekezo ya wakubwa wetu, tukae, tupange namna ya magavana wetu kushinda kwa kishindo halafu mmoja anatumzunguka na kwenda kutangaza hadharani, hatufai kabisa huyu...”


“Nimezungumza na mama, naona atakuwa amenisikia, lazima huyo mtu aondoke, anyang’anywe gari tulilompa na mshahara wake ukome kuanzia leo, naamini ‘chealedi’ atate-

keleza hili kabla ya jua halijachomoza,” alisema Mzee Tai kwa hasira.

Mzee huyo baadaye kidogo alihisi kuwa huenda “akaharibu zaidi,” alimgeukia mwandishi na kumuomba asiende kuyaandika aliyozungumza kwa kuwa yawezekana akawa anachochea moto kwenye nyasi kavu.

Mwandishi akamuomba samahani Mzee Tai kwa kumweleza kuwa mazungumzo hayo yali kuwa mubashara (live), hivyo hakuna namna ya kuyazuia kwani nayo yamefika kwa umma kama yalivyofika ya yule aliyekuwa akimlaani.

Tutumie tafsiri yako ushinde...



Huu ni mchoro wenye maana kubwa. Kila mmoja anaweza kuwa na tafsiri yake, hivyo gazeti la Pambazuko linatafuta tafsiri fupi, inayoelezeka na kufanua vyema kuliko zote na itachapishwa na gazeti hili kwenye Ukurasa wa 30 toleo linalofuata. Mhusika atatumiwa zawadi – Tuma tafsiri yako kwa simu: 0744 768 263.



Kumekucha Ngorongoro



Rais Samia Suluhu Hassan

Na Mwandishi WETU

KUMEKUCHA Ngorongoro! Ndivyo inavyoweza kuelezwa baada ya ahadi zilizotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa wakazi wa eneo hilo, kuanza kutekelezwa kwa kasi.

Baada ya maandamano ya siku sita ya wakazi wa eneo hilo, wakidai kurejeshwa kwa huduma za kijamii na haki yao ya kupiga kura, wiki iliyo-pita Rais Samia aliwatuma mawaziri waandamizi kutuliza wakazi hao kwa ahadi kuwa atatekeleza matakwa yao yote.

Mawaziri aliotumwa Ngorongoro na Rais Samia ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), William Lukuvi, aliyeambatana na Waziri Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi.

Ahadi hizo “ziliwapoza” wakazi hao ambao wengi wao ni wafugaji wa jamii ya Kimasai na wakarejea majumbani mwao kusubiri utekelezaji.

Pambazuko, baada ya kuanza kuandika habari za Tarafa ya Ngorongoro na kufuatilia kwa karibu, lilikutana na timu ya wataalamu wa kada mbalimbali walioagizwa na Ikulu, waliofika Tarafa ya Ngorongoro, Wilaya ya Ngorongoro, Arusha kuanza maandalizi ya kutimiza ahadi ya Rais Samia.

Timu hizo zilifika katika kata hiyo wiki iliyo-pita kwa ajili ya kuanza mandalizi ya urejeshwaji wa huduma za kijamii.

Pamoja na kutaka kurejeshewa huduma za jamii, ikiwamo maji, shule na vituo vya afya, wakazi wa Tarafa ya Ngorongoro walikuwa wakipinga majina yao kuhamishiwa Kijiji cha Msomera, Wilaya ya Handeni, Tanga kwa ajili ya kupiga kura kwenye uchaguzi ujao wa Serikali za Mitaa wakati wao bado wanaishi Ngorongoro.

Zaidi ya watu 9,000 kutoka tarafa hiyo walihamishiwa Msomera ikiwa ni kutekeleza mpan-go wa serikali kuhamisha watu kutoka Ngoron-goro – ikiwa ni kampeni ya kuokoa mazingira ya eneo hilo, na kuepusha uharibifu unaotokana na ongezeko la watu, mifugo na shughuli za kib-inadamu.

Akizungumzia na Pambazuko, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngoron-goro, Murtallah Mbillu, amesema kuwa kazi ya kurejesha huduma hizo tayari imeshaanza kwa kasi kubwa.

Amesema wataalamu wameshatembelea kata zote 11 zinazounda Tarafa ya Ngorongoro ili kuangalia maeneo yanayohitaji kufanyiwa kazi haraka.

Kwa mujibu wa Mbillu, ziara hiyo iliyofanyika kwa siku tatu kuanzia Agosti 26, mwaka huu, ilishirikisha wataalam mbalimbali ambao jukumu lao lilikuwa ni kutambua maeneo yenye changamoto zinazohitaji utatuzi wa haraka.

Alizitaja baadhi ya idara walikotoka wataalam hao kuwa idara za elimu, afya, maji, barabara pamoja na idara ya uchaguzi ambayo iliwakilishwa na ofisa wa uchaguzi ambaye alikuwa na jukumu la kubainisha maeneo yote yatakayotumika kupigia kura wakati wa uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajia kufanyika Novemba 27, mwaka huu.

“Kaka kama unavyojua rais akishaagiza kitu, huna muda wa kupoteza na tayari timu ya wataalam wetu imetembelea kata zote 11 zinazounda Tarafa ya Ngorongoro ili kuanza utekelezaji wa agizo la Rais Samia...”

Inaendelea Uk. 7

Kumekucha Ngorongoro

Inatoka Uk. 6

“Kimsingi, huduma za jamii Ngorongoro zili-kuwapo miaka yote, kwani kila mwezi zinapele- kwa shilingi milioni 29 kwa ajili ya huduma za jamii. Tatizo lililokuwapo ni kwamba, kwa miaka fulani fulani hapo nyuma, ili kutatua changamo- to iliyokuwa ikitokea katika taasisi za umma au eneo jingine lolote, ilikuwa lazima tuombe kibali kutoka Mamlaka ya Ngorongoro...”


“Lakini, kwa agizo alilolitoa mheshimiwa Rais Samia, sasa hatuhitaji kuomba kibali popote, ndiyo maana ninasema, afe kipa au afe beki, laz- ima huduma zirejeshwe haraka iwezekanavyo...”

“Kwa mfano, kuna baadhi ya shule zina chan- gamoto za vyoo, zingine zina changamoto za ma- jengo yake kuchakaa na kuna baadhi ya pampu za maji hazifanyi kazi na zimepelekea wananchi na wanafunzi kukosa maji ya uhakika...”

“Kwa hiyo, ili kutatua changamoto hizo, tuko tayari hata kubadilisha baadhi ya matumizi ya fedha zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya shu- ghuli fulani, ili zielekezwe katika utatuzi wa changamoto hizo ndani ya muda mfupi...”

“Ili kuhakikisha mambo yanakuwa sawa ndani ya muda mfupi, tumechukua ‘sola’ iliy- okuwa katika jengo la halmashauri na kuipele- ka katika maeneo yaliyokuwa na changamoto ya pampu za visima na pia tumeongea na watu wa Ruwasa, wakakague visima vyote vya maji ili vianze kutoa maji kwa kiwango kinachotakiwa huku tukiangalia pia kupeleka magari ya maji katika maeneo yote yaliyokuwa hayana maji ya kutosha,” amesema Mbillu.

Akisisitiza, alisema shule tatu za sekondari ambazo ni za bweni, mwaka jana ziliingiziwa shilingi bilioni 6.7 kwa ajili ya kuziendeleza na kwamba kama kuna changamoto ya huduma



Diwani wa Kata
ya Laitole, James
Moringe

za jamii katika halmashauri hiyo, ni za kawaida sawa na changamoto zinazopatikana katika hal- mashauri nyingine nchini...”

“Kwa hiyo, nawaomba wananchi wa Ngoron- goro watulie, wasiwe na wasiwasi kabisa kwani serikali yao iko kazini na kila kitu kitakuwa sawa siku si nyingi,” almeongea Mbillu.

Wakati mkurugenzi huyo akisema hayo, mad- iwani wawili wa tarafa hiyo walizungumza na Pamabzuko wamekiri kuwa kweli kuna maan- dalizi ya kurejesha huduma za jamii zilikuwa zi- mesitishwa katika tarafa zao kwa muda mrefu.


Hata hivyo, wakiongea kwa tahadhari, vion- gozi hao wa serikali za mitaa walisema kuwa kip- imo chao kitakuwa ni kurejeshwa kwa huduma hizo kwa ukamilifu na siyo maneno kutoka kwa viongozi.

Diwani wa Kata ya Laitole, James Moringe, amesema katika kata yake, timu hiyo ya wata- laam ilitembelea Shule ya Sekondari Laitole am- bayo chanzo chake cha maji kilikuwa kimehari- bika...”

Inaendelea Uk. 8



Habarika kidijitali! Soma gazeti la
Pambazuko na magazeti
mengine maarufu kwenye **Rifaly!**



Scan to download Rifaly

www.rifaly.com



Kumekucha Ngorongoro

Inatoka Uk. 7

“Kwa kifupi huduma za jamii zilikuwa zimesitishwa, ila sasa kuna maandalizi ya kuzirudisha kwani ile timu ya wataalam wa halmashauri ilitembelea Sekondari ya Laitole ambayo wanafunzi walikuwa wakichota maji kutoka Shule ya Wasichana Ngorongoro, baada ya chanzo cha maji kuharibika shuleni kwao...”

“Katika Sekondari ya Laitole, kuna sola zimepelekwa na wahandisi wameshafika shuleni hapo kukagua mazingira ya shule hiyo. ..”

“Pia, timu hiyo ya wataalam ilitembelea Shule ya Msingi Esole, ambayo nyumba mbili za walimu ziliezuliwa na upepo mwaka jana na pia walitembelea Zahanati ya Esole ambayo kwa muda mrefu ilikuwa inavuja...”

“Walifika pia katika Shule ya Msingi Oldoinyo ambayo choo chake kilikuwa kimedidimia na pia walikagua darasa moja lililojengwa kwa nguvu za wananchi, lakini halikuendelezwa kwa sababu ambazo serikali inazifahamu...”

“Kwa upande wa suala la uchaguzi wa Serikali za Mitaa, katika kata yangu, ofisa wa uchaguzi aliongeza vituo viwili vya kupigia kura, kimoja alikiweka katika Shule ya Msingi Oldoinyo na kingine katika Makumbusho ya Laitole...”

“Kwa hiyo, naweza kusema maagizo ya Mama (Rais Samia) yanatekelezwa kwa kasi kwa sababu hata ukiwaona hawa wataalam, wanaonekana wako serious (makini) na utekelezaji wa maagizo hayo,” ameingiza Moringe.

Katika Kata ya Enduleni, amesema wataalam hao walitembelea Shule ya Msingi Ndiani na Enduleni yenye watoto 1,876, matundu manane ya vyoo na majengo mawili ya mabweni ambayo hayajakamilika tangu mwaka 2021.

“Mabweni hayo ambayo ni ya wasichana na wavulana, zilitumika shilingi milioni 800 kuyajenga mwaka 2021, lakini ilipofika kwenye finishing (umaliziaji) yakasimama, ila kwa ujio wa hiyo timu, tunaamini yatakamilishwa kutokana na agizo la Rais Samia...”

“Wakati huohuo, Hospitali ya Kanisa Katoliki iliyoko Enduleni, tayari imeshapelekwa shehe-

na ya dawa na hadi sasa imeshaongezewa madaktari sita,” amesema Moringe.

Diwani wa Kata ya Ngorongoro, Saitoti Saimon, amesema kuna kila dalili kwamba huduma za jamii zitaanza kurejeshwa katika kata yake ingawa timu hiyo ya wataalam haikutembelea baadhi ya maeneo muhimu.

“Kuna kila dalili za mambo kwenda vizuri kwa sababu katika kata yangu, wataalam hao walitembelea shule tatu za msingi ambazo ni Makao Mapya, Oloilobi na Mokilali...”

“Katika Shule ya Msingi Oloilobi, walishuhudia choo kilichoanguka na kusababisha wanafunzi kukosa eneo la kujisaidia na katika Shule ya Msingi Mokilali, walitembelea choo kilichojaa na hivyo wanafunzi kukosa pia eneo la kujisaidia...”

“Kwa mujibu wa maelezo yao, ni kwamba vyoo hivyo vitajengwa upya ila nasikitika timu hiyo haikutembelea shule shikizi iliyoko katika Kitongoji cha Kayapsi ambayo haijakamilika ujenzi wake kwa miaka mitatu sasa na pia hawakutembelea shule shikizi iliyosimama ujenzi wake baada ya kampuni iliyokuwa ikijenga kunyimwa kibali cha kuingiza vifaa vya ujenzi.



Wakazi wa Ngorongoro. (Picha na BBC)

Mezani kwa Chahali

Na Evarist Chahali
evarist@chahali.com



Polisi inajinasua vipi kwa tuhuma za utekaji?



Kada wa Chadema, Deusdedit Soka

WIKI iliyopita ilitawaliwa zaidi na habari kuhusu watu watano ambao inadaiwa kuwa wametekwa, ingawa uthibitisho wake, bado unasuasua.

Watu hao ni makada wa Chadema, Deusdedit Soka, Jacob Mlay, Frank Mbise, Dioniz Kipanya na mchora vibonzo, Shadrack Chaula.

Watu hao wamepotea katika mazingira ya kutatanisha na hadi wakati safu hii inaandikwa, wali-kuwa hawajulikani walipo.

Viongozi na wafuasi wa Chadema pamoja na baadhi ya wanaharakati, wamelituhumu Jeshi la Polisi kuwa ndilo linawashikilia watu hao.

Kabla ya kupotea, Soka alidai kuwa alipokea ujumbe wa vitisho dhidi ya uhai wake. Kadhalika, kupitia akaunti zake kwenye mitandao ya kijamii, alitahadharisha kwamba Jeshi la Polisi lilikuwa linamwinda.

Kwa upande wa Chaula, awali alikamatwa na kufunguliwa mashtaka kwa kosa la kuchoma picha ya Rais Samia Suluhu Hassan, kabla ya wanaharakati na wananchi mbalimbali kuhamasishana

na kufanikiwa kupata kiwango cha fedha kilichohitajika ikiwa ni faini baada ya kuhukumiwa. Fedha hizo zilipatikana na hatimaye aliachiwa huru.

Lakini licha ya watu hao watano, takwimu zilizotolewa na Chadema zinadai kuwa zaidi ya watu 100 wamepotea katika mazingira ya kutatanisha sehemu mbalimbali nchini.

Na katika mkutano wake na waandishi wa habari hivi karibuni, Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe aliwapa fursa baadhi ya jamaa za waliopotea kuzungumza na waandishi wa habari na kupaza sauti kuhusu kupotea kwa jamaa zao.

Wanasheria kadhaa walifungua kesi dhidi ya baadhi ya viongozi wa ngazi za juu wa Jeshi la Polisi kuwataka, aidha wawafikishe mahakamani Soka na wenzake au kuwaachia huru.

Hata hivyo, mahakama ilitoa uamuzi kwamba waleta mashtaka wameshindwa kuthibitisha kuwa watu hao waliopotea, wako mikononi mwa jeshi hilo.

Awali, wanasheria husika walidai kuwa wana ushahidi wa “fuso (malori) mbili” kwamba Polisi ndiyo inawashikilia Soka na wenzake, lakini hai-kuweza kufahamika endapo ushahidi huo ulitupiliwa mbali au haukuwepo.

Kwa bahati mbaya, japo matukio ya watu kupotea yaliwahi kutawala huko nyuma, hakujawahi kufanyika jitihada za makusudi kuchunguza chanzo cha matukio hayo, wahusika na hatua za kuhakikisha hayajirudii.

Inakumbukwa kuwa kada maarufu wa Chadema, Ben Saanane alipotea Novemba mwaka 2016 na hadi leo, siyo tu haifahamiki kilichomsibu, bali pia hakuna mtu yeyote aliyechukuliwa hatua.

Lakini siyo tatizo la watu kupotea tu ambalo halijapatiwa mwarobaini. Mwezi huu ni miaka saba kamili tangu Makamu Mwenyekiti wa Chadema Taifa, Tundu Lissu anusurike kuuawa baada ya shambulio la risasi, lakini hadi sasa waliofanya shambulio hilo haijawahi kuelezwa jitihada za vyombo vya usalama kuwasaka, hivyo hawajafahamika.

https://instagram.com/evarist_chahali



Tafakuri ya Bagonza

Mihimili ikioana, itazaa 'mazingeta'

Na Dkt. Benson BAGONZA

TUHUMA na malalamiko kuhusu uhuru wa mihimili zinaongezeka kila siku nchini mwetu. Na hii haikuanza jana wala juzi. Yamekuwepo miaka mingi. Mihimili hiyo ni Bunge, Mahakama na Serikali.

Hata ndani ya mihimili yote kuna malalamiko yanayoibuka kila uchao. Kila mhimili unalilia uhuru. Kuna kilio cha kutaka kuwa huru zaidi na zaidi na kujipa nafasi ya kuamua.

Tatizo ni pale mhimili mmoja unapokuwa na tamaa ya kuuoa mwingine. Tatizo la pili ni pale mhimili mwingine unapotamani kuolewa. Hapa lazima waathirika watakuwa ni watoto wa mihimili hii kwa pamoja.

Tuache mchezo. Kuna nchi, ikigundulika rais alimpigia simu jaji mkuu kumpa heri ya siku yake ya kuzaliwa (Happy Birthday), inatosha kupeleka hoja bungeni kuanza kumjadili kumunda madarakani - "Impeachment process".

Akitaka kumtakia heri jaji mkuu au jaji yeyote, sharti afanye kwa uwazi hata gazetini na vyombo vya habari vitangaze, umma ujue na kusiwepo na uficho wa kufanya hivyo. Uhuru wa mihimili siyo jambo la kuchezea!

Hata watoto wa wakuu wa mihimili wakioa-

na, yaweza kusababisha taharuki nyingine kubwa yenye kuweza kusababisha madhara.

Naheshimu uhuru wa kukusanyika na kujieleza. Uhuru huo unasaidia kuonyesha ujinga wetu ili tusaidiane kuufuta na kusimama mahali pazuri zaidi.

Hakuna aliye salama mihimili ikioana. Dhuluma, rushwa, ukatili, biashara, uwekezaji, usalama wa mitaji, hata mifumo yote itasambaratika.

Nchi hii ni kubwa na muhimu kuliko chama chochote, chombo chochote na mtu yeyote. Wote tunahitaji uhuru wa mihimili.

Hata washenga wa ndoa ya mihimili, kama watapatikana, wataanza kuichukia ndoa hiyo mara baada ya kuwa imeshafungwa.

Tuhuma za mihimili kuoana au kufungishwa ndoa ya mkeka zisipuuzwe. Ukianza kuona walalamikaji hewa ujue kuna wafungwa hewa na majaji hewa.

Mihimili hii ndugu waliozaliwa na baba na mama mmoja. Hawaruhusiwi kuoana (Incest). Ni kosa na halipaswi kufanyika ili umma uendelee kustawi.

Ni vyema na busara kila mhimili ukakaa peke yake na kusiwepo hata chembe ya matamanio ya kuwa na ndoa.

Kila mmoja ukae peke yake. Hata kutongoza na hawaruhusiwi.

Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Jimbo la Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.





Hoja Yangu

Na Rashid MTAGALUKA

Matusi mitandaoni, mamlaka za udhibiti zimeshindwa kazi?

KATIKA dunia ya kidijitali, mitandao ya kijamii imekuwa sehemu muhimu ya maisha ya watu wengi, hata hivyo pamoja na faida zake nyingi, kumekuwa na changamoto kubwa ya kuongezeka kwa matumizi mabaya ya mitandao.

Wengi wanatumia mitandao hiyo kwa matusi, kejeli, na lugha ya chuki. Swali linalojitokeza ni hili, je, mamlaka za udhibiti zimefanikiwa kudhibiti hali hii au zimeshindwa kabisa?

Ileweke kuwa mitandao ya kijamii inajumuisha mamilioni ya watumiaji wanaochapisha maudhui kila sekunde, na pengine kuna marika tofauti; wakiwamo watoto wadogo na hata wazee. Pia jinsi tofauti; wake kwa waume.

Katika mitandao hiyo, faragha imekuwa ikiingiliwa na umma kushuhudia yasiyopaswa kuwa hadharani yanasambaa.

Ninafahamu kuwa zipo sheria za kudhibiti maudhui ya mtandaoni katika nchi nyingi, ikiwa ni pamoja na adhabu kali kwa wanaokutwa na hatia ya kueneza lugha ya chuki au matusi mtandaoni, lakini bado uhalifu huo unaendelea kukomaa.

Hali hiyo inapoendelea kukomaa na kuota mizizi, inaleta hofu kwa umma kwamba huenda mamlaka zinazopaswa kudhibiti hazifanyi kazi zake sawasawa, ndiyo maana matukio ya matusi yanaendelea kuongezeka.

Pamoja na kuwepo kwa sheria, utekelezaji wake umekuwa ukisuasua. Watu wengi wanaoeneza matusi hawachukuliwi hatua za kisheria, na hili linaweza kuwakatisha tamaa waathirika.

Aidha, katika baadhi ya matukio, mamlaka zinashindwa kuchukua hatua kwa sababu ya maslahi ya kisiasa au ushawishi wa watu mashuhuri ambao mara nyingi hawachukuliwi hatua za kisheria.

Nimalizie hoja yangu wiki hii kwa kusema kuwa, ili kudhibiti matusi kwenye mitandao, ni muhimu kwa mamlaka za udhibiti kuchukua hatua madhubuti zaidi za kubaini wanaotenda

makosa na kuchukua hatua kali zaidi.

Kwanza kuimarisha utekelezaji wa sheria zilizopo ambazo zinapaswa kutekelezwa kwa nguvu zote, bila kujali hadhi ya mtu au ushawishi wake.


Jambo jingine ni kuanzisha kampeni ya kutoa elimu kwa Umma, kwa kufanya kampeni za uelewa kuhusu madhara ya matusi mtandaoni. Kampeni hizi zinapaswa kuimarishwa, na watu wafundishwe jinsi ya kutumia mitandao kwa njia ya heshima na inayowajibika.

Aidha, ushirikiano na kampuni za mitandao unapaswa kuhimizwa na mamlaka za udhibiti ilikuwa na nguvu kubwa zaidi za kukomesha hali hiyo.

Pia mamlaka zinapaswa kushirikiana kwa karibu na kampuni za mitandao ya kijamii ili kuhakikisha kuwa sera za kukabiliana na matusi zinatekelezwa ipasavyo.

Ni muhimu kwa jamii kutambua kuwa matumizi mabaya ya mitandao yana madhara makubwa na kila mtu ana wajibu wa kuhakikisha kuwa mitandao inatumika kwa manufaa ya wote.

Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546 na email; mtagaluka@gmail.com



Na Godwin CHILEWA,
Houston

Kurunzi la Intelijensia

Nafasi za uongozi zizingatie taaluma

Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dkt.
Stergomena Tax akiwa amegeuza darubini

NAHESHIMU sana Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayompa rais mamlaka ya kuteua viongozi na wasaidizi anaowataka.

Naheshimu majukumu ya viongozi na nafasi walizopewa na kwa namna yoyote siyo nia yangu kumshambulia au kumkebehi mtu kwa chuki au sababu binafsi. Lengo langu ni kutoa maoni yenye nia ya kujenga.

Hivi karibuni niliona picha ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Stergomena Lawrence Tax akiwa na Rais Samia Suluhu Hassan kwenye shughuli ya mafunzo ya kijeshi.

Picha hiyo inamuonesha Stergomena Tax akiwa anaangalia mazoezi hayo akiwa amegeuza kiona mbali (darubini) iliyopaswa kumuwezesha kuona vizuri na kwa ukaribu. Nashawishika kuamini kuwa alikuwa hajui kifaa hicho kinatumiwaje. Natamani angeuliza.

Swali ambalo wadau wengi wanajiuliza ni kama waziri huyo alifanikiwa kufuatilia mazoezi hayo ipasavyo, na baadaye kuweza kutoa maoni yake; kuwapongeza, na au kubadilishana mawazo na makamanda au Rais Samia kuhusu yale aliyoyaona.

Binafsi simlaumu Tax kwa kugeuza kiona mbali, maana mtu yeyote ambaye hajawahi kutumia kifaa hicho angeweza kufanya hivyo. Hata

hivyo, ninasikitika kwamba huyu ndiye waziri anayeshughulika na makamanda na wapiganaji wetu.

Ni kwa sababu hii nadhani kuna haja kubwa kwa Rais Samia akaangalia kwa makini nafasi anazowapa wateule wake kama zinaendana na taaluma zao hata kama watu hao wana elimu ya juu au uzoefu wa mambo mengine.

Sina shaka hata kidogo kuhusu elimu na uzoefu wa uongozi wa Stergomena Tax. Nafahamu ana shahada kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, na shahada ya juu kutoka Chuo Kikuu cha Tsukuba, Japan. Siyo hivyo, tu huyu ana uzoefu wa kutosha wa mambo ya utawala na diplomasia. Kwa kifupi anafaa sana kuwa waziri wa mambo ya nchi za nje.

Nisisitize hapa kwamba wizara ya ulinzi ni mojawapo ya wizara nyeti kabisa inayohusisha usalama wa mipaka, ustawi wa makamanda na wapiganaji, silaha na mafunzo.

Mambo haya yanaweza kufanywa kwa weledi zaidi na mtu mwenye uzoefu na jeshi hususan jenerali mstaafu au aliyepo madarakani.

Hata kama hatuna wanajeshi wastaafu ambao sasa ni wanasiasa, rais anaweza kumteua jenerali au kanali mstaafu kuwa mbunge na kisha kumkabidhi wizara ya ulinzi.

Mara nyingi tunajidanganya kwamba uwaziri ni nafasi ya kiutawala na usimamizi wa sera tu. Sivyo! Kuna zaidi ya hilo. Wenzetu kwenye nchi zilizoendelea huthamini sana taaluma, na ni nadra kuona wizara kama ya ulinzi anapewa mtu ambaye hajawahi kuwa ofisa wa juu wa jeshi. Hili hufanyika kwa kujua tabia na utamaduni wa jeshi.

Suala hili linapaswa kuzingatiwa pia kwa wizara nyingine za kipekee. Kwa mfano, itakuwa kichekesho kukabidhi wizara ya sheria kwa mtu mwenye shahada ya uhandisi majengo, na wizara ya mipango na uchumi kwa daktari wa mifupa.

Mwandishi ni mchambuzi wa masuala ya intelijensia, na mwandishi wa vitabu. Anaishi Houston, Texas, Marekani.

Kona ya Dkt. Bisimba

Na Dkt. Hellen Kijo
BISIMBA

Kuchaguliwa Dkt. Ndugulile kumeliinua taifa

NCHI yetu niliifahamu kama nchi nzuri yenye watu wema, ukiilinganisha na nchi nyingi za jirani, za bara la Afrika na hata za dunia ya tatu na pengine hata ulimwenguni.

Ninafahamu kuwa kama nchi, tuliweza kupokea wakimbizi kutoka karibu kila nchi iliyo jirani nasi na hata mbali kama Afrika Kusini na Zimbabwe.

Nchi yetu ilianza kupata dalili zisizo njema polepole na kwa sasa nionavyo mimi hali ya kujivunia haipo tena, kwani kila kukicha utasikia vilio vya waliopotelewa na ndugu na watoto, kwa kutekwa au vinginevyo.

Vyombo vya habari vimejaa vilio vya makundi mbalimbali wakiwamo wakazi wa Ngorongoro wanaolalamikia kuhamishwa kwa nguvu, Si-manjiro wanawake wanaolia kukosa huduma ya maji kwa muda mrefu, mikataba mibovu inayotishia uendelevu wetu kama nchi - kwa kutaja vilio vichache.

Katika yote hayo kuna watu wamejaribu kuikimbilia mifumo ya utawala waki-tarajia kupata nafuu, lakini napo na-fuu haijaonekana.

Waliokwenda Polisi kutoa taarifa ya kutekwa au kupotelewa na ndugu, wamepokea majibu yasiyoridhisha wengine wakiambiwa huenda hao wamejiteka.

Waliojaribu kuikabili Mahakama, nako wamepewa majibu ya kiushahidi, waliokimbilia bungeni spika mwenyewe kasema haoni kama ni jambo la kipaumbele kujadiliwa na Bunge.

Kidogo wananchi walioamua kuandamana na kuweka kambi kudai haki zao huko Ngorongoro walisikika na viongozi kwenda huko ingawaje hatuna uhakika kama ahadi walizopewa zinatupa-

tia suluhisho la kudumu.

Basi, kati ya haya yaliyo hasi tumepokea angalau taarifa chanya iliyotufurahisha kama nchi. Nili-jifunza kuwa wakati hali ikiwa mbaya na msongo wa mawazo, ukiwa mkubwa ni vyema kutafuta kitu au jambo lililo la kufurahisha uliinue zaidi ili kuua msongo.

Tulipopata habari kuwa Mtanzania amepata kazi kubwa ya kimataifa katika Shirika la Afya Duniani (WHO), niliona labda tulichukue hili kama jambo chanya kati ya haya mambo ya maumivu na vilio ili litusaidie kujenga uchanya katika kutafakari na kutafuta njia za kukabiliana na adha na dhiki zinazoendelea nchini.

Kwa hali hiyo, ninawiwa kuungana na Watan-zania wengine kumpongeza Dkt. Faustin Ndugul-ile, aliyechaguliwa kuwa Mkurugenzi wa WHO Kanda ya Afrika. Ni Mtanzania wa kwanza kushi-ka nafasi kubwa kama hii.

Dkt. Ndugulile ameinua furaha yetu kama nchi tukijitazamisha kuwa kumbe kuna vitu vizuri vinavyoweza kuonekana kati yetu, tena katika kipindi hiki cha mashaka.

Sifa za Dkt. Ndugulile ni nyingi na ni wazi amepata nafasi hii kwa uwezo wake mkubwa huo na ameonyesha vipaum-

bele nane ambavyo atashughulikia akiwa kazini katika wadhifa wake mpya, ikiwemo kushughulikia afya ya uzazi na watoto, magonjwa yasiyoambuki-za, afya ya msingi na hata usalama wa kiafya.

Tunampongeza kwa kupata wadhifa huo lakini pia tunampongeza kwa kutuini-lia jambo chanya katikati ya mambo hasi yaliyotugubika na kutukwamisha kama Taifa.

Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwanaharakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatikana kwa namba 0713 337240.





Ana kwa Ana

Dkt. Slaa: Samia alidharau ushauri wangu kuhusu ‘ugaidi’ wa Mbowe

KATIKA toleo lililopita, tulianza kuchapisha mahojiano maalum na Katibu Mkuu (wa zamani) wa Chadema, Dkt. Willibrod Slaa. Alieleza mambo mengi kuhusu historia na mwanzo wa harakati zake za “kupigania haki.” Sehemu hii ya pili anaelezea namna anavyoshiriki siasa licha ya kusema kuwa ameachana na siasa za vyama za majukwaani. Endelea...

Pambazuko: Kujiuzuku kwa makamu mwenyekiti wa CCM, Abdulrahman Kinana, je, ni hasara au mtaji kwa chama hicho?

Slaa: Mimi nitafurahi ikiwa ni hasara kwa CCM. Wakija CCM kuniomba ushauri sitaki. Siwezi kuwa na uhusiano na chama chenye tuhuma nyingi za mauaji.

Sativa yuko wapi? Kimempata nini? Huyu mama (Samia Suluhu Hassan) angekuwa rais mwenye roho, angethubutu kupeleka milioni 35 behind the scenes (nyuma ya pazia) badala ya yeye kwenda Aga Khan kumuona na kumuuliza; “mwanangu nini kimekupata: - halafu akachukua hatua.

Inatokea mtu anapigwa risasi, anakwenda kutupwa halafu na watawala hawachukui hatua zozote. Unawezaje kufanya hivyo?

Sativa ametupa somo kubwa sana. Mungu ana jambo la kumfundisha Samia. Samia anapaswa kujifunza katika tukio la Sativa.

Angalia suala la yule kijana wa Tanga. Mtu anapotea siku nyingi, polisi wanakana kumshikilia, lakini baadaye wanampeleka mahakamani huyohuyo ambaye walisema hawamshikili.

Huyu Samia nilimpigia simu wakati alipofanya mahojiano na (Salim) Kikeke wa BBC, wakati ule akasema Mbowe (Freeman – mwenyekiti wa Chadema) na wenzake watatu eti wameshafungwa kwa ugaidi.

Nilimpigia simu nikamwambia mama umepotoshwa, hakuna mtu aliyefungwa. Wale uliosema wamefungwa kesi yao imeisha na wako mitaani.

Ukitangaza kuwa ni magaidi wamefungwa, unazuia watalii kuja kwa hofu.

Akaniambia niongee na mwanasheria wake, nikaongea naye akampelekea ujumbe wangu. Samia



Dkt. Willibrod Slaa

akamwambia mwanasheria aniambie nimwandikie kwenye Whatsapp, si email tena.

Nikamwandikia kama kurasa tatu, nikimshauri nini cha kufanya ili kurekebisha hilo, baada ya muda akanipigia simu akaniambia niongee na msaidizi wake.

Sasa nikashangaa, msaidizi na mwanasheria ni nani anayestahili kushughulikia suala kama hilo. Nadhani ni mwanasheria.

Mbowe akakaa gerezani miezi minane na hatimaye wakamtoa. Kama iliwezekana kumtoa baada ya miezi minane, kwa nini kilishindikana kumtoa mwanzoni?

Mtu amewekwa ndani, ameteseka muda wote huo!

Huyu ndiye mnataka mimi niende kuongea naye? Niongenee naye nini?

(Pambazuko lilimtafuta Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Amos Makalla kujibu tuhuma za chama chake kuwa kinabeba wauaji, akasema; “kamwe CCM hakiwezi kuwa na wala hakihusiki na mauaji, ni chama makini kinachopigania haki, maendeleo na ustawi wa Tanzania na watu wake.”)

Pambazuko: Unazungumziaje mgogoro wa Chadema na wabunge 19, wakiongozwa na Halima Mdee?

Slaa: Hili ni suala la Chadema wenyewe kuamua. Kama wanaona inafaa kuwasamehe, wawasamehe waendeleo kujenga chama.

Hata kama walikosea, lakini hata katika Biblia inaelezwa kuwa hakuna kosa lisilosameheka. Kama yule aliyetundikwa na Yesu msalabani alisamehewa,

Dkt. Slaa: Samia alidharau ushauri wangu kuhusu ‘ugaidi’ wa Mbowe

Inatoka Uk. 14

sembuse hawa.

Mimi sitaki kuwahukumu watu.

Pambazuko: Tangu tumeanza mfumo wa vyama vingi matokeo ya kura za vyama yanashabihiana na yale yaliyotolewa na ile tume ya kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi, yaani asilimia 80 – kwa CCM na 20 kwa wapinzani, je, kwanini hali iko hivyo?

Dkt Slaa: Haya matokeo unayapata wapi? Kwenye tume wanaficha. Wanaficha kwa sababu matokeo yote ni manufactured (yanatengenezwa). Mimi nili-wakamata live (mubashara).

Nilipiga kura Karatu, nikarudi hapa. Kuna mtu wa Geita akanishtua ananiuliza kama nafuatilia matokeo, nikamwambia hapana.

Akaniambia fuatilia kwa sababu kwenye kituo chetu wametangaza kuwa umepata sifuri na Kikwete amepata 3,000 wakati matokeo waliyobandika ukutani bado yapo, wewe hukupata hizo. Wewe ndio ume-pata 3,000 Kikwete sifuri.

Kwenye kituo kingine ulipata 15,000 mjini Geita, Kikwete amepata kura 300, lakini matokeo yametangazwa kinyume.

Ni wizi. Tunaibiwa kura.

Kuna baadhi ya vituo inaonekana matokeo yanafanana. Yanafanana kwa sababu katika kituo kimoja kunaweza kuwa na vituo vidogo kama saba au nane. Wakiona unamshinda wanatengeneza vituo hewa.

Na hili tumelikuta mahakamani mimi na Tundu Lissu. Wameniiibia kwa namna ambayo sisi hatukugundua.

Kila tukijumlisha tunapata namba sahihi, lakini wao walipoenda mahakamani idadi ya kura zinazoletwa ni tofauti kwa sababu wanaongeza na zile za vituo hewa.

Hilo lilituchanganya sana. Baadaye nikaanza kupitia mwenyewe zile document (nyaraka) za mahakamani nikakuta kuna karatasi zina vituo viwili tofauti jina la msimamizi ni lililile. Nikaangalia matokeo nikakuta kituo kimoja kipo mbali na mjini, hii ya kwanza nimepewa sifuri, mtu wao amepata 300.



Katibu Mkuu wa zamani wa Chadema, Dkt. Willibrod Slaa (kushoto), akizungumza na Mhariri Mtendaji wa Pambazuko, Peter Nyanje wakati wa mahojiano maalum nyumbani kwake jijini Dar es salaam. (Picha Fidelis Felix)

Kwenye fomu ya pili, yenye namba ileile original (halisi) ya tume, ile ya kituo bandia mimi nimepata 300 lakini wamefuta.

Wana njia mbalimbali za kuiba. Kuna hiyo ya kufuta ili mfanane au wanafuta ili kumpandisha mwenzako.

Wanazalisha vituo bandia, lakini si wa kule wilayani, ni hapa hapa (Dar es Salaam).

Pambazuko: Kwa hiyo yale madai ya kutaka kujua karatasi na nyaraka za uchaguzi zimechapishwa wapi ni ya msingi?

Dkt. Slaa: Ndio maana walinichukia nilipotangaza nina taarifa kuna gari limetoka Afrika Kusini na shehena ya karatasi za kura. Wakati huo mimi najua karatasi za kura zimechapishwa Kalamazoo ya Uingereza.

Asubuhi msimamizi wa uchaguzi na polisi wakanusha badala ya kuniuliza niwape taarifa zaidi. Lakini wao wakanikandika.

Lakini mimi nilipata kwa watu wa immigration (Uhamiaji) na watu wa customs (forodha) walioko bandarini, kwa sababu walikuwa ni wapenzi wangu.

Usiku uleule wale watu waliitwa Dar es Salaam na

Inaendelea Uk. 18

Uchaguzi Marekani



Kura za maoni zamshusha Trump, Harris ang'ara



Makamu wa Rais wa Marekani, Kamala Harris

Na Mwandishi WETU

BAADA ya vyama vikubwa nchini Marekani; Democrat na Republican, kukamilisha uteuzi wa wagombea wao, sasa kampeni za uchaguzi mkuu zimepamba moto.

Kama ilivyo kawaida, taasisi kadhaa nchini humo zimeanza kukusanya takwimu za kura za maoni ili kupima kukubalika kwa wagombea katika ngazi mbalimbali.

Kabla ya uteuzi wa wagombea na kabla ya kujitoa kwa aliyedhaniwa kuwa atakuwa mgombea wa Democrat, Rais Joe Biden, kura za maoni zilikuwa zinaonyesha kuwa mgombea wa Republican, Donald Trump, alikuwa anaongoza kwa kura nyingi za maoni.

Lakini mambo yamebadilika na kugeuka ghafla, baada ya Biden kujiondoa kwenye kinyang'anyiro na Democrat kumteua makamu wa Rais, Kamala Harris, kupeperusha bendera ya chama hicho.

Hivi sasa kura za maoni zinaonyesha kuwa mwanamama huyo amempiku Trump na kuon-

goza.

Jambo hilo limeanza kuitisha timu ya kampeni ya Trump kwani mambo yamegeuka ghafla sana, kinyume cha matarajio yao.

Kugeuka kwa takwim hizo kumeonekana kupitia kura za maoni zilizofanywa na PolCom Lab na Mainstreet Research USA, taasisi kubwa zinazoheshimika kwa kazi hiyo.

Pamoja na mambo mengine kura hizi zinaonyesha mgawanyiko mkubwa kutokana na jinsi na rangi ya mtu miongoni mwa wapiga kura nchi nzima.

Kura hizo zinaonyesha kuwa kitaifa Harris amechukua uongozi mbele ya rais wa zamani Trump. Wakati asilimia 47 ya wapiga kura wakisema kuwa watamchagua Harris, asilimia 43 tu ndio waliobainisha kuwa wao wanapendezwa zaidi ya Trump.

Hizo ni kura zilizopigwa kwa wananchi wote bila kujali kama watapiga kura au la.

Ukiangalia kura za maoni zilizofanyika miongoni mwa watu ambao wamehakikisha kuwa watapiga kura, matokeo yanaonyesha kuwa bado Harris anaongoza kwa asilimia 49 huku Trump akiwa na asilimia 45.

Matokeo yanaonyesha kuwa Harris anaungwa mkono kwa wingi na wapiga kura wanawake ambao asilimia 53 wamesema wanamuunga mkono huku asilimia 45 ya wanaume nao wakionyesha kuvutiwa na mgombea huyo.

Kwa upande mwingine, Trump anaungwa mkono na wanaume wengi, asilimia 47, ikilinganishwa na asilimia 41 ya wanawake wanaomuunga mkono.

Harris pia anaongoza kupendwa na wapiga kura weusi (asilimia 73), watu wenye asili ya Hispania (asilimia 51) na wazungu ambao wana elimu ya kuanzia chuo kwenda juu (asilimia 57).

Kwa upande wa Trump, anaendelea kuungwa mkono kwa wingi na wapiga kura wazungu ambao elimu yao ni chini ya ngazi ya shahada ya chuo kwa asilimia 59.

"Tangu ateuliwe kupeperusha bendera ya Democrat, Makamu wa Rais Harris amekuwa kipenzi cha wapiga kura wanawake na tofauti ya kijinsi imekuwa dhahiri," anasema Dkt. Luzmari-



Kura za maoni zamshusha Trump, Harris ang'ara

Inatoka Uk. 16

na Garcia, Profesa msaidizi kutoka Chuo Kikuu cha Florida Atlantic (FAU).

Anaongeza: “Harris pia ameimarisha mizizi ya chama cha Democratic miongoni mwa wapiga kura kutoka katika makundi ya watu wachache.”

Harris pia ameonyesha kumpiku Trump miongoni mwa wapiga kura ambao hawana vyama. Katika kundi hili Harris anaongoza kwa asilimia 48 kulinganisha na asilimia 35 ya wanaomuunga mkono Trump.

Hali hii inaonyesha mabadiliko makubwa ikilinganishwa na hali ilivyokuwa mwezi Julai, mwaka huu ambapo wapiga kura wasio na vyama walikuwa kama wamegawanyika nusu kwa nusu, huku asilimia 45 wakimuunga mkono Harris na asilimia 43 wakiwa nyuma ya Trump.

Kwa ngazi za chini, kura zinaonyesha kuwa asilimia 46 ya wapiga kura watampigia kura mgombea wa chama cha Democrat katika wilaya zao ikilinganishwa na asilimia 44 watakaomchagua mgombea wa chama cha Republican.

“Kwa ujumla matokeo haya yanaonyesha jinsi nchi ilivyogawanyika. Inaonyesha kuwa uchaguzi huu utakuwa na mpambano mkali sana,” anasema Profesa msaidizi na mkurugenzi mwenza wa Pol-Com Lab, Kevin Wagner.

Mgawanyiko kihisia

Kura hizo za maoni zinaonyesha kuwa kuna mgawanyiko mkubwa kihisia miongoni mwa wapiga kura huku wale wa hisia hasi wakiwa juu kwa asilimia 44 dhidi ya asilimia 41 ya wenye hisia chanya.

Mgawanyiko huu wa kihisia unaonekana dhahiri pale unapoanishwa na dhamira inayowasukuma wapiga kura hao.

Katika kundi hili, wanaomuona Harris kwa mtazamo chanya ni asilimia 52, huku asilimia 35 kwakimuona kwa mtazamo hasi.

Kwa upande wa Trump, asilimia 34 wanamtazama kwa mtazamo chanya huku asilimia 49



Donald Trump

kwakimchukulia kwa mtazano hasi.

Kwa ujumla, asilimia 27 ya wanachama wa Democrat wanaonyesha kusisimkwa sana na uchaguzi, huku asilimia 32 ya wanachama wa Republican wakisema kuwa wana hofu ya uchaguzi huo.

Wanachama wengi wa Democrat wameonyesha kufurahishwa na timu ya wagombea wao, Harris na Tim Walz, aliyeteuliwa na Harris kuwa mgombea mwenza.

Misimamo ya wagombea

Katika misimamo ya kisiasa, Harris na mgombea mwenza wake, Gavana wa Minnesota, Tim Walz, wao wanaonekana kuwa na siasa za mreno wa kushoto.

Harris anaonekana kuwa ni mtu aliyeegemea sana mreno wa kushoto (asilimia 37), kulinganisha na Walz (asilimia 28).

Hata hivyo, Walz anaonekana kama mtu asiye na misimamo mikali, huku asilimia 18 ya wapiga kura wakimuona kama mtu mwenye misimamo ya kati.

Kwa upande wa Republican, Trump na mgombea mwenza wake, JD Vance, wanaonekana kuwa wa mreno wa kulia, huku Trump akionekana kama mwenye misimamo mikali ya mreno wa kulia (asilimia 37) na Vance kwa asilimia 30.

Vyama

Asilimia 46 ya Wamarekani wameonyesha kufurahishwa na jinsi chama cha Democrat kinavyofanya shughuli zake wakati asilimia 38 wao hawafurahishwi na chana hicho.

Hata hivyo, pengo linaongezeka zaidi ukifanya mlinganisho wa kuridhika miongoni mwa wanachama, huku asilimia 64 wanachama wa Democrats wakionyesha kuridhishwa na chama chao, ikilinganishwa na asilimia 33 ya wanachama wa Republican.



Ana kwa Ana

Dkt. Slaa: Samia alidharau ushauri...

Inatoka Uk. 15

asubuhi wakafukuzwa kazi, kwa hiyo wizi mkubwa sana wa kura unafanyika very systematically (kimfumo).

Mimi sikuishia hapo, niliwauliza Kalamazoo kwa sababu hawataki kampuni yao iingie kwenye dosari, wakaniambia sisi karatasi zetu zina security features (alama za usalama) na wakanitajia hizo security features.

Pambazuko: Lakini safari hii wanasema wanataka kuchapisha karatasi za kura hapahapa.

Dkt. Slaa: Si watafanya wizi mkubwa. Kwani sisi ni mara ya kwanza tunawakamata hapa?

Hivi unajua wanapochapisha sheria ndogondogo, sijafanya utafiti wa sheria kubwa, lakini wanapochapisha sheria ndogondogo wanakwenda wanablock number, lakini document (nyaraka) haichapishwi, inaweza kuchapishwa hata mwaka kesho.

Nikiwa kwenye kamati ya kudumu ya bunge ya sheria ndogondogo tukabaini kuwa sheria nyingi ndogondogo hazijachapishwi kwa wakati huo.

Pambazuko: Nini kilikushawishi kukubali kazi ya ubalozi wakati ndio kwanza ulikuwa umetoka upinzani?

Dkt. Slaa: Mimi ni mwanasheria, mimi ni mwanasiasa. Mimi naelewa systems (mifumo) zinafanyaje kazi duniani. Inabidi utenganishe kazi za serikali na kazi za chama.

Serikali ni utumishi, moja kati ya heshima kubwa kwa mtu ni kuaminiwa kufanya kazi serikalini.

Bahati mbaya sisi Tanzania tunachanganya hatuoni tofauti kati ya siasa na utumishi wa umma. Naelewa kwa hiyo haikunipa shida.

Ukipewa utumishi wa umma wa level (ngazi) hiyo, ni heshima sana.

Siku ananiapisha Rais Magufuli (John - awamu ya tano) aliweka hadharani kuwa – “tume kuwa na marafiki zetu Sweden, hivyo nataka uende kurudisha yale mahusiano kwa sababu Sweden ni nchi ya Kikristu, wewe umekuwa Baraza na wale umefanya nao kazi, nenda ukarudishe yale mahusiano.”

That is what I did (hicho ndicho nilichofanya). Na mpaka leo bado wananipigia simu. Hata kama

Magufuli tunamsema kwa mambo yasiyo mazuri, lakini na yeye ana mazuri yake, na tukarudisha mahusiano.

Pambazuko: Kabla Rais Magufuli hajakutangaza kuwa Balozi, alikushirikisha? Au na wewe ulisikia tu kwenye vyombo vya habari kama sisi?

Dkt. Slaa: Alinishirikisha dakika tano kabla hatatangaza. Alinipigia simu, sikuwa na namba yake kwenye simu yangu kwa hiyo sikujua.

Nilipopokea sikujua sauti, kama alinificha sijui, lakini sikutambua.

Akaniambia; hujambo, nikajibu sijambo. Akasema siyo kwamba naomba kibali chako, ninakuambia kwa sababu sitaki tugombana nawe kwenye vyombo vya habari. Nimekuteua.

Pambazuko: wakati huo alikuwa ameshajitambulisha?

Dkt. Slaa: Ndio alijitambulisha maana nilimuliza wewe ni nani akaniuliza dokta, hunitambui Magufuli? Aaah hapana, hakuniambia Magufuli, aliniliuliza; Baba Askofu hunitambui? Na kwa kuwa tulishazoea yeye kuniita kwa jina hilo tangu tukiwa bungeni, aliponiita hivyo tu nikamtambua.

Lakini hakuniambia ameniteua kwa nafasi gani, akakata simu. Inaonyesha hakuwa anataka mazungumzo au mjadala kuhusu hilo.

Dakika chache baadaye ndio nikaanza kupokea pongezi kutoka kwa rafiki zangu wakinipongeza kwa kuteuliwa kuwa balozi.

Pambazuko: Na kama angekujulisha mapema ungekataa?

Dkt. Slaa: Hapana, nisingekataa kwa sababu mimi nilikuwa nimeshaondoka kwenye siasa na huu ni utumishi wa umma. Nani anakataa utumishi wa umma.

Kitu pekee ambacho kilinitisha ni kuwa aliniteua nje ya umri wa utumishi wa umma. Lakini mimi ni mwanasheria najua kuwa kada hiyo ilianzishwa na Marekani miaka 20 iliyopita.

Pambazuko: Unamwelezeaje Magufuli?

Dkt. Slaa: Magufuli lazima umgawe katika mafungu mawili. Magufuli ana mambo mabaya linapokuja suala la siasa. Siku zote tunamjua hivyo, hajawahi kuwa mzuri kwenye mambo ya demokrasia, hata ubunge wake alivyopata tunajua. Jinsi alivyo mtoa aliyekuwa mpinzani wake Phares Kabuye, mambo aliyoyafanya ni mabaya.

Inaendelea Uk. 19



Dkt. Slaa: Samia alidharau ushauri...

Inatoka Uk. 18

Mimi mwenyewe najua mambo aliyoyafanya Karatu, alinikata miguu kabisa. Aliwahi kuja Karatu kuandaa ziara ya Mkapa, halafu Mbunge sikujulishwa.

Lakini nilikutana naye wakati anafanya maandalizi nikamwambia sitakuwepo wakati wa ziara kwa sababu nilikuwa na safari ya Kibunge kwenda kwenye mkutano wa SADC.

Baadaye Mkapa alipokuja alizungumza kwenye mkutano, mimi sikuwepo na Magufuli akawaambia watu kuwa mbunge wenu alijua kuwa rais anakuja huku yeye ametoroka.

Anayasema haya wakati anajua kuwa nilikuwa safari ya SADC niliyotumwa na Bunge.

Niliporudi nikaenda bungeni moja kwa moja. Siku moja Magufuli akaja akakaa karibu na kiti changu akaniambia Baba Askofu nimekuja kuungama. Nikashangaa. Nikakaa mkao wa kuungamisha, akaniambia nisamehe nimekuharibia sana wakati wa ziara ya Mkapa, ile ahadi niliyokupa mbele ya wananchi nimekwenda kinyume.

Akaniuliza; hivi ulitegemea mbele ya rais wangu nikusifie?

That is Magufuli (huyo ndiye Magufuli). Alikuwa anakutendea ubaya, lakini baadaye anakiri kwako na kuomba msamaha.

Alikuwa hana rafiki. Hata siku moja usitegemee uharibu kazi halafu Magufuli akutetee. Mimi niliipenda hiyo.

Hakuwa mtu anayependa masihara kwenye kazi, habembelezi mtu.

Kwenye wizi kuna watu wamezusha amekutwa na bilioni 42, ni uongo. Wale ni watu wasiomjua Magufuli. Magufuli ilikuwa kila senti inayoingia inakwenda kufanya kazi.

Nayajua haya kwa sababu amenishirikisha.

Kwenye SGR mathalan, hakutaka mawaziri watoke nje, yeye mwenyewe alikuwa hatoki nje, kwa hiyo sisi mabalozi ndipo tulikuwa tunamsaidia kutafuta fedha za ujenzi wa SGR.

Mtu hawezi kutafuta hela kwa njia hiyo halafu aingize mfukoni kwake.

Kumbuka tulizuiwa misaada kutokana na kauli za Makonda (Paul – akiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam) kuhusu ushoga. Nimekwenda nimepiga magoti tukafunguliwa.

Kwa hiyo Magufuli kuna mambo anafanya vizuri lakini kuna baadhi ya wasaidizi wake walikuwa wanamdanganya kwenye baadhi ya mambo na kusababisha yeye kufanya maamuzi yasiyo sahihi. Kwa mfano suala la kuzuia mikutano ya vyama vya siasa baada ya uchaguzi.

Pambazuko: Unalionaje Bunge la sasa? Unadhani linatimiza wajibu wake sawasawa?

Dkt. Slaa: Kuna Bunge? We unaniulizaje swali kama hilo? Liko wapi? Lilichaguliwa na nani?

Maana ya Bunge ni nini? Anza na tafsiri maana ya Bunge ni nini. Bunge ni chombo cha uwakilishi. Lakini hili limechaguliwa na wananchi?

Kati ya mambo mabaya ya Magufuli ni hayo. Mimi Magufuli aliniomba niende Karatu kuisaidia CCM. Nikamkatalia, akaniomba mara ya pili, nikakataa na mara ya tatu, nikiwa Balozi. Sasa alipofika Karatu akaenda akasema uongo. Nimeongea na Balozi wenu amenituma, akanilisha maneno.

Pambazuko: Lakini hata kama wabunge hawakupatikana kwa njia sahihi, lakini Bunge kama taasisi lina majukumu yake.

Dkt. Slaa: Kisheria wapo, si wameapishwa? Lakini katika macho ya wananchi je?

Kweli Bunge ni taasisi, lakini taasisi inaundwa na watu. Kama watu ni wazuri, basi taasisi itakuwa nzuri na kama watu ni wabaya, basi hata taasisi yao itakuwa mbaya tu. Hauwezi kuwa na taasisi nzuri inayoundwa na watu wabaya, haiwezekani hata siku moja.

Na ndio kuna mfano nautoaga kwa CCM siku zote. Ndio maana watu hawanielewi. CCM kama CCM nikiisifu ni kwa sababu ina mambo mazuri. Tatizo ni watu waliomo CCM, si CCM.

Hata CCM ni taasisi nzuri sana, lakini wale walio mo ndani yake ndio wanasababisha CCM ionekane kuwa ilivyo hivi leo.

Pambazuko: Nini sasa kifanyike ili tuwe na taasisi ya Bunge ambayo inafanya kazi ambayo inapaswa kuifanya kwa ajili ya Watanzania?

Dkt. Slaa: Ni katiba tu. Mimi sitaki kuzungukazu-nguka, suluhisho ni kuwa na Katiba nzuri na iheshimike.



Matumizi ya rada yang'arisha Tanzania



Na Andrew MSECHU

MABORESHO sekta ya hali ya hewa Tanzania yameshika kasi na kuendelea kuipa heshima, huku ikiaminiwa kutoa mafunzo na ujuzi kwa nchi zingine.

Mapinduzi katika sekta hiyo yanadhihirika kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kuaminiwa kusimamia mafunzo ya kuwajengea uwezo wataalamu wa eneo hilo kutoka nje ya Tanzania.

Mafunzo ya hivi karibuni kufanywa na TMA yaliwahusisha wataalamu kutoka taasisi za hali ya hewa Afrika na Kitengo cha Elimu na Mafunzo cha Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO).

Mafunzo hayo mahsusi ya matumizi ya data na taarifa za rada za hali ya hewa yaliyomalizika mwishoni mwa wiki jijini Mwanza kwa usimamizi wa TMA.

Katika ufunguzi wa mafunzo hayo, Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, alisema lengo kuu la mafunzo hayo ilikuwa ni kuimarishwa zaidi kwa uwezo wa wataalamu wa hali ya hewa na wajuzi wengine wanaohusiana na sekta hiyo kutoka baadhi ya nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika.

Alisema mafunzo hayo yalilenga zaidi matumizi bora ya taarifa za rada za hali ya hewa kwa ajili ya kuboresha utabiri wa hali ya hewa na

utoaji wa tahadhari za matukio ya hali mbaya ya hewa kwa jamii.

“Mafunzo haya ni sehemu ya utekelezaji wa mpango ulioasisiwa na Umoja wa Mataifa wa utoaji wa tahadhari mapema kwa wote ifikapo mwishoni mwa mwaka 2027 na sera ya WMO ya kubadilishana data za hali ya hewa kimataifa,” alisema.

Prof. Mbarawa alisisitiza umuhimu wa kufanya uwekezaji wa miundombinu ya kisasa ya hali ya hewa kama vile rada, akifafanua kuwa Tanzania imekuwa kilelezo bora katika kufanya uwekezaji huo pamoja na kuwajengea uwezo wataalamu wa hali ya hewa nchini, hivyo kuchochea fursa ya kuandaa mafunzo hayo.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMA na Mwakilishi wa kudumu wa WMO, ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Jopo la Kimataifa la Sayansi ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi, Dkt. Ladislaus Chang'a, alieleza kuwa TMA imejipanga vyema kupitia wataalam wake kutoa mafunzo ya aina hiyo kila yanapohitajika.


“Wataalam walioandaliwa kwa ajili ya kutoa mafunzo ni wabobezi, baadhi yao wamepata mafunzo kutoka Marekani na Finland na vilevile ni wakufunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam,” alisema Dkt. Chang'a.

Mwakilishiki kutoka WMO (Ofisi ya Mafunzo), Eunjin Choi, aliishukuru Tanzania kwa kufanikisha mafunzo hayo muhimu ya matumizi ya taarifa na data za rada za hali ya hewa ili kuendeleza malengo ya kuboresha huduma za hali ya hewa, siyo tu kwa Tanzania, bali duniani kote.

Nchi wanachama za WMO zilionufaika kwa mafunzo hayo ni Tanzania ni Burundi, Comoro, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Kenya, Msumbiji, Malawi, Mauritius, Rwanda, Shesheli, Sudan Kusini, Uganda, na Zambia.



Habarika kidijitali! Soma gazeti la Pambazuko na magazeti mengine maarufu kwenye Rifaly!



Scan to download Rifaly

www.rifaly.com



ODM kusimama au kumeguka bila Raila?

Na Julious MKAMBI, Nairobi

SERIKALI ya Kenya chini ya uongozi wa Rais William Ruto, imejitosa – siyo tu, kumuunga mkono kiongozi wa upinzani, Raila Odinga kuwania Uenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika (AUC), bali pia kumfanyia kampeni.

Mwanzoni mwa wiki iliyopita, Rais Ruto aliongoza viongozi wa Afrika Mashariki akiwemo Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan katika uzinduzi wa kampeni za Raila kumrithi Mousa Faki wa Chad kwenye uchaguzi wa Uenyekiti AUC utakaofanyika Februari mwakani.

Tangu Raila atangaze nia kuwania enyekiti huo, wapo waliofurahia wakiona majukumu hayo mapya yatamweka nje ya siasa za Kenya, na pia wapo waliopinga kwa madai taifa litakosa mtu makini wa “kupiga darubini” utendaji wa serikali.

Kwa muda mrefu, Raila ameonakena ndiyo sauti ya upinzani kiasi kwamba akiitisha maandamano nchi nzima, mwitikio unakuwa mkubwa, lakini matukio ya hivi karibuni yakiongozwa na vijana wa Gen Z, yamedhihirisha hata bila ya uwepo wa Raila, wananchi wanafahamu haki zao.

Raila ametangaza ‘kustaafu’ siasa za Kenya akijipanga kulitumikia Bara la Afrika akiwa na imani atakuwa mrithi wa Faki na hii imesababisha kuibuka maswali mengi kuhusu hatma ya Chama cha Orange Democratic Movement (ODM) ambacho yeye ndiye kiongozi wake.

ODM ni moja ya vyama tanzu ndani ya muungano wa vyama vya upinzani, Azimio la Umoja, lakini uamuzi wa chama hicho kutoa viongozi waandamizi kuteuliwa na Rais Ruto kwa nyadifa za uwaziri, kimekiweka njia panda.

Hali kama hiyo pia inashuhudiwa ndani ya ODM ambapo baadhi ya wanachama hawajafu-



Waziri Mkuu wa zamani wa Kenya, Raila Odinga

rahishwa na kitendo cha chama hicho kushirikiana na serikali na pia Raila kuwania Uenyekiti wa AUC.

Raila alipotangaza nia ya kumrithi Faki, viongozi waandamizi wa ODM walianza kuvutana kuvaa viatu vyake kukiongoza chama hicho kongwe cha upinzani nchini Kenya.


Miongoni mwa viongozi hao ni waliokuwa manaibu wa Raila; Hassan Ali Joho na Wycliffe Oparanya.

Lakini wawili hao walijiiondoa baada ya Rais Ruto kuwateua mawaziri, huku viongozi wengine waandamizi wa ODM waliopewa uwaziri wakiwa ni pamoja na Mwenyekiti John Badi na Kiongozi wa Wachache Bunge la Taifa, Opiyo Wandayi.



Kenya

ODM kusimama au kumeguka...



Rais wa Kenya, William Ruto



Uzoefu hauji na umri, unakuja na changamoto ulizozikabili. Naweza kuwa nina miaka 35, lakini nimekumbana na kutatua changamoto kibao..."

2022.

Tangu mwaka 2007, chama tishio na chenye ushawishi mkubwa kimekuwa ODM kutokana na uongozi thabiti wa Raila, lakini sasa anapojiweka pembeni na siasa za Kenya, akisaka uenyekiti wa AUC je, chama hicho bado kitakuwa imara au ndiyo kitasambaratika?

Mbunge wa Embakasi Mashariki ambaye pia ni kijana na mwenye ushawishi mkubwa, Babu Owino, ametangaza nia yake ya kumrithi Raila akisisitiza amepitia changamoto nyingi kwenye safari yake kisiasa, hivyo ameiva kwa nafasi hiyo.

Babu ni miongoni mwa wanasiasa ndani ya ODM ambao - japo anamheshimu Raila na kumsifu kutokana na mchango wake wa dhati kukuza demokrasia ya Kenya, anapinga kitenendo cha viongozi waandamizi wa chama hicho kukubali uteuzi wa Rais Ruto wa kuunda serikali ya pamoja.

Mbunge huyo anasema Raila amekuwa kiongozi wake kisiasa akiwa amefanya kazi chini yake na sasa Raila anapoondoka, amejitangaza yuko tayari kuwa kiongozi wa upinzani na kuhakikisha ODM inabaki imara.

"Uzoefu hauji na umri, unakuja na changamoto ulizozikabili. Naweza kuwa nina miaka 35, lakini nimekumbana na kutatua changamoto kibao..."

"Wengine wanaweza kuwa wameishi muda mrefu, lakini hawajakumbana na mitihani," alisema Babu.

Ni dhahiri wanasiasa wengi kama Babu watajitokeza kumrithi Raila, lakini kikubwa ni hatma ya chama cha ODM bila kiongozi huyo wa siasa za Kenya, aliyepachikwa jina la 'Baba.'

Inatoka Uk. 21

Tayari ODM imetangaza watakaochukua nafasi za walioteuliwa mawaziri na sasa inasubiriwa kuona nani atakayevaa viatu vya Raila ili kuendelea kulisukuma gurudumu la ODM na kujipanga kwa uchaguzi mkuu wa mwaka 2027.

Siasa za Kenya kwa muda mrefu zimetegemea ushawishi au umaarufu wa mwanasiasa kuliko chama, ndiyo kwa maana tangu chama cha KANU kiondolewe madarakani kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2002, hakuna chama kimeweza kutetea uchaguzi wa urais na kushinda peke yake.

Mwai Kibaki alishinda urais uchaguzi mkuu wa mwaka 2002 kupitia jumuiko la vyama la NARC na kufanikiwa kutetea nafasi yake ya urais miaka mitano baadaye kupitia chama cha PNU wakati Uhuru Kenyatta alipochaguliwa Rais mwaka 2013 alifanya hivyo kupitia TNA ambacho kiliungana na vyama vyingine kuunda muungano wa Jubilee.

Kenyatta alivishawishi vyama tanzu kwenye muungano huo vijivunje na kuunda chama kimoja cha Jubilee alichokitumia kutetea nafasi yake ya urais kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka

Mkuu wa Wilaya ya Longido atumbuliwa

Na Mwandishi WETU

MKUU wa Wilaya ya Longido, mkoani Arusha, Mariko Henry Ng'umbi, jana ilikuwa siku yake ya mwisho kuwa kiongozi wa ngazi hiyo baada ya kuhudumu kwa siku 579.

Ukomo wake umetokana na kutenguliwa kwa uteuzi wake na Rais Samia Suluhu Hassan kupitia tarifa fupi iliyosambazwa na Ikulu jana.

Pamoja na kwamba taarifa ya Ikulu haikutaja sababu za kuondolewa kwa dhamana ya ukuu wa wilaya kwa Ng'umbi, lakini Pambazuko linaweza kueleza pasi na shaka kuwa ameondolewa kwa "kufichua" alichoita mwenyewe mbinu za ushindi wa madiwani wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa Wilaya ya Longido.

Ng'umbi (pichani) anatamba katika picha jongefu (video fupi) kwenye mitandao ya kijamii kwamba "ni serikali ndiyo iliwafanya wakapita bila kupinga katika uchaguzi wa mwaka 2020."

Katika video hiyo fupi, Ng'umbi ambaye anaonekana kuzungumza na madiwani wa CCM, anawaeleza kuwa bila "mbinu za serikali," wao wasingekuwa viongozi.

Ng'umbi akaongeza; "Diwani huna ujanja wowote wa kushinda, bila serikali, ndiyo maana hata sasa hivi, sisi tumeshafanya kuchakata hali ya mambo."

Pambazuko lilimtafuta Ng'umbi, kueleza endapo anayozungumza yanahusika kwenye maandalizi ya uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu? Hakupatikana, kwani simu zake zote zilithibitika kuzimwa.

Ng'umbi aliapishwa kushika wadhifa huo wa ukuu wa wilaya Januari 31, 2023 na jana Septemba 1, 2024 alitenguliwa.

Ng'umbi anaungana na aliyekuwa waziri wa Habari, Mawasiliano, Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, ambaye Julai 21, mwaka huu alitenguliwa kwa kutoa kauli inayoendana na ile aliyoitoa mkuu huyo wa wilaya.



Wabunge CCM kuchuja wagombea EALA leo

Na Mwandishi WETU

MCHAKAMCHAKA wa kusaka wawakilishi wa Tanzania ndani ya Bunge la Afrika Mashariki, umeanza ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Jana, chama hicho tawala, kilianza mchakato wa kuwapata wagombea wake na kutangaza majina 10 ya waliopitishwa kuwania nafasi za ubunge huo.

Waliochaguliwa, leo watakuwa "wakichambuliwa na Kamati ya Wabunge wa CCM" kabla ya kuamua nani wapelekwe ndani ya Bunge la Jamhuri kwa ajili ya kumpata mwakilishi.

Katika kikao chake kilichoketi jana jijini Dar es Salaam, Kamati Kuu Maalumu ya CCM, ilitangaza kuwateua makada wake 10 kugombea

nafasi ya ubunge wa Afrika Mashariki (EALA), kurithi nafasi iliyoachwa wazi na Dkt. Shongo Sedoyeka aliyefariki dunia Juni 13, 2024.

Wajumbe wa kikao hicho, walikata majina ya makada wengine 37 walioweka nia ya kuomba ridhaa kwa kutuma majina yao kwa ajili ya kuteuliwa "kujaribu bahati zao."

Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM, Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Amos Makalla alisema jana baada ya kikao hicho kuwa majina yaliyopitishwa "yameonekana kukidhi matamano ya CCM."

Aliwataja walioteuliwa ni Gladness Salema, Maria Sebastian, Queenelizabeth Makune, Ester Chaula, Profesa Neema Kumburu, Lucia Pande, Fatuma Kange, Hawa Mkwela, Fatma Msofe na Theresia Dominic.

Septemba 5, mwaka huu, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania litamchagua mmoja kuwa mwakilishi wa Tanzania ndani a EALA.



Mtoto wa Mvuvi

Na Maregesi PAUL



Sasa Mungu aingilie kati kukomesha utekaji



Vitendo vya utekaji

TAARIFA za utekaji wa watu, zimekuwa ziki-shika kasi kila kunapokucha.

Watu wengi wamekuwa wakilalamika watoto, ndugu, marafiki kutekwa ama kupotea katika mazingira ya kutatanisha kila uchao.

Yaani, leo ukipata taarifa za watu kadhaa kutekwa wakiwa katika shughuli zao za kila siku jijini Dar es Salaam, Mwanza na Arusha, kesho usishangae kusikia idadi fulani ya watu wametekwa katika mikoa ya Tanga, Pwani, Mbeya na kwingineko nchini.

Kwa ujumla, watu wanalalamika na kibaya zaidi, Jeshi la Polisi, ambalo ndilo lenye jukumu la kuwalinda raia na mali zao, linalalamikiwa kila

kona kwa kile kinachoelezwa kwamba halichukui hatua za dhati kukabiliana na uharifu huo.

Dar es Salaam wanalilalamikia jeshi hilo, Mtwara wanalinyooshea kidole, Mara, Dodoma, Katavi na kwingineko nchini, lawama ni zile zile, kwamba Jeshi la Polisi linahitaji kuongeza kasi ya kukabiliana na utekaji huo ambao unalifanya li-onekane haliwajibiki ipasavyo.

Kwa kuwa Polisi inaonekana kukwama kukabili hali hiyo, sasa tumebakiwa na chaguo moja tu, nalo ni kila mmoja sasa kumuomba Mwenyezi Mungu - Muweza wa yote, afanye kila analoweza kutuepusha na kadhia hiyo ambayo inatukosesha usingizi Watanzania.

Wanaosali makanisani, ibada zao ziwe ni kuke-mea uhalifu huo, wamwambie Mungu jinsi tuna-vyuumizwa na matukio hayo, wamweleze Muumba wetu huyo jinsi utekaji unavyochukiwa na kila mmoja wetu.

Pia wasisahau kumwambia Mungu kwamba yeye ndiye Muweza wa yote na ndiye mwenye uwezo wa kuleta heri na neema kwa Watanzania kwa kukomesha utekaji.

Wasiishie hapo, wamwambie pia jinsi Jeshi la Polisi la nchi yetu linavyolalamikiwa kila kona ya nchi hii kwa sababu ya uhalifu huo na wasisahau kumwambia kwamba, njia pekee ya kulinasua jeshi hilo katika lawama hizo, ni Yeye Muumba kuingilia kati kwa kuwaongezea maarifa askari wetu.

Halafu Mungu awajaze moyo wa utu na utalamu unaohitajika utakaowapa njia sahihi za kukabiliana na uhalifu huku wakiwakamata na kuwafikisha katika vyombo vya dola wote wanaotuhumiwa kwa utekaji wa watu.

Waislam nao wasijiweke kando, wanapoingia misikitini wakati wa kukamilisha swala, maombi yawe ni yaleyale, wamwambie Mwenyezi Mungu, kwamba Watanzania wamechoshwa na utekaji wa watu na sasa wamejikabidhi mikononi mwake.

Wasiokuwa na dini, nao wafanye matambiko yao kadiri wanavyoweza.

Naamini yote haya yakifanyika utekaji wa watu ambao unalaaniwa na kila mmoja wetu, Mungu ataingilia kati na kukomesha utekaji ambao unalititia doa taifa letu na kuliondolea sifa zake zenye mizizi miaka nenda -rudi.



Dkt. Ndugulile aonya...

Inatoka Uk. 4

“Nampongeza sana Dkt. Ndugulile kwa kuipeperusha vyema bendera ya Tanzania. Naamini atakwenda kuongoza vizuri ikizingatiwa Afrika ina matatizo mengi.

Kutokana na taaluma yake na uzoefu, naamini atakwenda kuyaweka sawa,” amesema Profesa Tibaijuka.

Akitoa uchambuzi wake kuhusu ushindi huo wa Dkt. Ndugulile, mwandishi wa habari za sayansi na mhariri wa gazeti la MwanaSayansi, Dkt. Syriacus Buguzi, amesema mkurugenzi huyo mpya wa WHO Kanda ya Afrika anakwenda kuitumikia Afrika kwa ujumla na afahamu kuwa akishindwa itakuwa sawa na kushindwa kwa Tanzania.

“Hii ina maana kwamba kwa mara ya kwanza, Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla, imetoa kiongozi atakayekuwa kwenye nafasi nyeti ya kuamua kiuongozi kuhusu hatua muhimu za kupambana na maradhi na kuboresha afya ya jamii. Akishindwa na Tanzania imeshindwa. Akifanikiwa na Tanzania imefanikiwa...”

“Kuhusu anapaswa kufanya nini, nadhani vipaumbele vya WHO kwa upande wa Afrika viko wazi, lakini yeye ameinisha kwenye kampeni zake jinsi atakavyotimiza malengo ya nchi zetu za Afrika na shirika katika kuboresha huduma za afya...”

“Kitu cha muhimu ni kupambana kuleta matokeo hasa kwenye kukabiliana na vifo vinavyotokana na magonjwa ambayo yanazuilika,” ameongeza Dkt. Buguzi.

Kuanzia mwakani atakaposhika rasmi nafasi hiyo pengine Dkt. Ndugulile atalazimika kuhamia Congo-Brazaville, yaliko makao makuu ya WHO Kanda ya Afrika.

Ataitumikia nafasi hiyo kwa kipindi cha miaka mitano na baada ya muhula wake wa kwanza, atakuwa pia na haki ya kuwania muhula wa pili.

Ushindi wa Dkt. Ndugulile unatokana na kuungwa mkono na Rais Samia Suluhu Hassan ambaye Mei 8, 2024 alitoa hotuba ya kumuunga mkono na kumpigia debe katika kinyang'anyiro hicho.

Dkt. Ndugulile anakwenda kuiwakilisha Afrika, bara linalokabiliwa na uhaba wa vifaa tiba, vifo vya uzazi huku kwa upande wa Watanzania wakikabiliwa pia na changamoto kubwa katika matumizi ya bima

ya afya.

Dkt. Ndugulile pia ana changamoto ya kupambana na athari za kiafya zitokanazo na mabadiliko ya hali ya hewa, upatikanaji mdogo wa huduma za afya, kupungua kwa usaidizi wa wafadhili, magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza.

Uchaguzi ulivyokuwa

Dkt. Ndugulile ambaye ni mtaalamu wa afya ya umma, alikuwa mmoja wa wagombea watano waliojitokeza kurithi mikoba ya Dkt. Matshidiso Moeti anayemaliza muda wake.

Dkt. Moeti, raia wa Botswana amehitimisha muhula wake wa pili akiwa Mkurugenzi wa Kanda wa WHO, katika kikao cha 74 cha Kamati ya Kanda ya Afrika ya WHO kilichofanyika nchini Congo Brazzaville wiki iliyopita.

Dkt. Ndugulile alikuwa akishindana na Dkt. Boureima Hama Sambo wa Niger, Dkt. Richard Mihigo wa Rwanda, Dkt. N'da Konan Michel Ya wa Ivory Coast na Dkt. Ibrahima Socé Fall wa Senegal.

Kura zilipigwa na mawaziri wa afya kutoka Kanda ya Afrika walioanza katika mkutano uliofunguliwa na Rais wa Congo, Denis Sassou Ng'uessou.

“Tutasimamia kujenga mifumo ya afya imara, tunaona mifumo mingi imeathirika kwa vita na majanga mengine zikiwemo mvua za El -Nino,” alisema Dkt. Ndugulile katika kampeni zake.

Muda mfupi baada ya Dkt. Ndugulile kutangazwa kuwa mshindi, Rais wa Samia Suluhu Hassan alituma pongezi zake kupitia ukurasa wake mtandao wa X akisema msomi huyo ameifanya Tanzania kuwa fahari sambamba na Bara la Afrika.

“Nina imani kwamba ujuzi wako na uzoefu wako katika sekta ya afya, utaiwezesha Afrika kuwa na sauti muhimu katika ngazi ya kimataifa kukabiliana na changamoto za afya kwa mamilioni ya watu wetu katika bara,” aliandika Rais Samia.

Spika wa Bunge, Dkt. Tulia Ackson, alisema; “kwa niaba ya Bunge nampongeza Dkt. Ndugulile kwa kuchaguliwa kuwa mkurugenzi wa WHO. Kazi nzuri zaidi imefanyika kwa maana ya kampeni.”

Agosti 23, 2024 akihojiwa na mtangazaji Mohamadou Houmfa wa Sauti ya Amerika (VOA), Dkt. Ndugulile alisema kilichomsukuma kugombea nafasi hiyo ni kwa sababu nchi nyingi bado hazijafikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG) ya 2030, hivyo anaamini ataleta kila kitu kinachohitajika kwa kazi hiyo mezani.



Onyo: Hakuna mafanikio kupitia miujiza ya dini



Mhadhili wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Mwenyekiti Chama cha Wanasaikolojia Tanzania, Dkt. Shagembe Magolanga.

Na Arodia PETER

KUNDI la Watanzania ambao wanaamini kuwa matatizo yao ya kiuchumi, kifamilia, ndoa na uhusiano yatamalizwa kupitia miujiza inayofanywa na viongozi wa kidini ‘wa kizazi kipya’ – wanajidanganya.

Wanaoonekana kushabikia na hata kuamini mafanikio ya miujiza, wengi wakiwa wanawake, wameshauriwa kutumia njia zenye uhalali wa kisayansi, ikiwamo kufanya kazi.

Watu wengi wanakimbilia kwa viongozi hao wa kidini waliochipuka nchini kama uyoga wakivutiwa na imani kuwa matatizo yao yatataliwa na watu hao.

Tanzania na nchi nyingine za Afrika Mashariki zinashuhudia kuwapo kwa wimbi kubwa la viongozi wa dini waliojipa vyeo mbalimbali; ikiwamo manabii, mitume, wachungaji, makuhanani na maaskofu, ambao wanamiliki makaniisa mbalimbali maarufu, huku badhi wakiita makanisa yao, ‘vituo vya maombezi’.

Lakini baadhi ya manabii na mitume wanalalamikiwa na jamii kuwa wanatumia vibaya Neno la Mungu kwa kugeuza huduma hizo kuwa sehemu ya kujinufaisha kiuchumi.

Tafiti za watu mbalimbali wakiwamo wanasaikolojia, viongozi wa dini na wasomi wanaelezea mambo yanayosababisha kuwapo kwa hali hiyo.

Mhadhili wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Rais wa Chama cha Wanasaikolojia Tanzania, Dkt. Magolanga Shagembe, anasema kisaikolojia watu wengi wanaamini kuwa dini ni kitu ambacho ni suluhisho na inaweza kumsaidia kutatua matatizo yanayomkabili katika maisha yake.

Anasema wengi wanaamini kuwa dini ina uwezo na nguvu kuliko uwezo wao wa ndani wa kufanya mambo.

Msomi huyo alibainisha kuwa wale wanaoamini katika dini za Kiafrika, wapagani na wanaoamini katika dini za kubwa za Ukristo na Uislamu, wote wapo kwenye mtazamo mmoja linapokuja suala la imani ya dini zao.

“Hawa wote wanatafsiri mambo yao katika imani; ndiyo maana wakipata changamoto za kiuchumi, ndoa, uhusiano na familia wanahusisha na imani zao...”

“Mpagani anaweza kufikiri amekosea kwenye matambiko yake, Mkristo au Muislamu anaweza kuhusianisha changamoto zake na uchawi, mila na hata ‘mapepo,’” anasema.

Dkt. Shagembe, ambaye ni mtalaam mbobevu wa saikolojia ya jamii, anasema imani mara nyingi inatokana na binadamu kwa namna alivyoyumbwa na kulelewa, kila mmoja anajitahidi kuhakikisha anakuwa na maisha mazuri, lakini tafsiri ya maisha mazuri inatofautiana mtu mmoja na mwingine...”

“Wengine wanadhani wakienda kwa waganaga wa kienyeji au wachungaji watafanikiwa haraka,” anasema.

Kuhusu wanawake kuvutwa kwa wingi kutafuta miujiza kuliko wanaume, Dkt. Shagembe anasema jinsia zote zinahusika katika kutafuta miujiza isipokuwa wanaume wanakwenda kwa kujificha tofauti na wanawake ambao ni wepesi kujitokeza waziwazi kuelezea shida zao...”

Onyo: Hakuna mafanikio kupitia miujiza ya dini

Inatoka Uk. 26

“Kwa muktadha wa kisaikolojia, wanawake ni majasiri, wana ujasiri wa kujitokeza waziwazi mbele ya watu kueleza shida zao kitu ambacho wanaume hawawezi kukifanya kirahisi. Wanaume kwa namna walivyolelewa ni watu wa kupambana...”

“Katika mila za kiafrika changamoto zote za kifamilia zinaangukia kwa mwanamke. Hata usaliti wa ndoa, mwanaume anaweza kukamatwa ugoni zaidi ya mara moja, lakini ndoa ikaendelea kuwepo tofauti na mwanamke akihusika kwenye usaliti wa ndoa ni nadra sana kusamehewa,” anasema Dkt. Shagembe.

Nini kifanyike

Mtaalam huyo wa saikolojia ya jamii, anashauri kuwepo usimamizi wa mamlaka kwa watoa huduma wote wa masuala ya imani za kidini ili kuhakikisha wanafuata taratibu, sheria na miongozo iliyowekwa ikiwa ni pamoja na kulinda hadhi na utu na kuhakikisha kuwa huduma hizo hazitumiki kuwaumiza watu kwa maslahi binafsi ya wanaozitoa.

“Pia vyombo vya habari na taasisi mbalimbali tuendee kupaza sauti ili watu wajue si kila changamoto yao inatokana na kulogwa, nguvu za giza au mapepo. Kuna baadhi ya matatizo yanaweza kutatuliwa na wataalamu wengine kama vile wa saikolojia, ustawi wa jamii na afya ya akili.

“Wakati mwingine shetani unaweza kuishi naye ndani, shetani ni yale mawazo na fikra zako mbaya. Nashauri tuwekeze pia kwenye tafiti kujua ni kwa nini watu wameelekeza fikra kwenye kutafuta miujiza,” anasema Dkt. Shagembe.

Askofu Bagonza: Ni msongo wa mawazo

Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Karagwe, Kagera, Dkt. Benson Bagonza, anasema sababu kubwa ya kuongezeka kwa watu wanaokwenda kufuata miujiza kwa ‘manabii’ na ‘mitume’ ni pamoja na

kuongezeka kwa msongo wa mawazo miongoni mwa wanajamii wengi.

“Wanawake ni wahanga wakubwa kwa saba-bu ya power structure (mifumo ya utawala) inayowafanya waonekane watu wasio na mamlaka au nguvu katika jamii...”

“Kwa hiyo, wanakwenda kutafuta miujiza ili kuziba ombwe la kukosa mamlaka na madaraka katika jamii inayowaona ni binadamu daraja la pili,” anafafanua.

Askofu huyo anasema kuwa manabii pia ni waathirika wakubwa wa msongo wa kiuchumi, kwa hiyo wanawatumia watu wenye msongo mkubwa wa mawazo ili kujinufaisha kiuchumi...”

“Ndiyo maana hakuna nabii anajenga shule, hospitali wala kuwapa maji hao maskini. Wote wanajenga majumba, mahoteli, wanamiliki magari ya kifahari ili kuziba ombwe la matamnio ya kiuchumi...”

“Theory (nadharia) ya pili ni unasaba kati ya dini na umaskini. Penye dini nyingi kuna umaskini na penye umaskini sana kuna dini nyingi. Kwa nini? kwa sababu dini ni social control (mdhibiti wa kijamii) ya kutuliza maskini wasiasi. Pia ni tiba ya kuwapa matumaini,” anasema Askofu Bagonza.

Ili kuepukana na haya yote, Askofu Bagonza anashauri kuongezwa kwa juhudi za kupambana na umasikini kwa kutumia elimu na si kuondoa umasikini kwa kuondoa uhaba wa vitu.

“Serikali ndiye mteja mkuu wa manabii kwani inawatumia kugawa sauti za wana dini. Lakini watumishi wa serikali ndiyo waumini wa dini hizo. Serikali yetu haina dini na haina suluhisho la hakika. Labda kutunga sheria inayodhibiti ukusanyaji wa fedha,” anasema.

Inaendelea Uk. 30



Mchungaji Richard Hananja



Riwaya

Viaticum-4

Sakramenti ya Mwisho



Dola za Marekani

Na GodChilewa

KATIKA sehemu ya tatu, tuliona namna tiketi ya ndege ilivyoleta iliyotumwa kwa Eddy ilivyoleta mvutano na mgongano wa mawazo. Endelea kujua nini kinafuata...

Sasa tatizo liko wapi hapo? Zaidi ya yote mtu huyo amekutumia pesa za kutosha kwa matumizi ya safari. Tena katika dola!

Huoni kama huyu ni mtu wa maana sana kwako?" Stella alieleza kwa upole na ufasaha mkubwa kama mama anayembembeleza mwanawe anayeugua maralia akubali kuchomwa sindano.

"Dada yangu, hayo uliyosema yote niliyafikiria mara tu baada ya kusoma huu ujumbe. Tatizo leo ni Jumatano na misa yenyewe ni Ijumaa asubuhi..."

"Ina maana kwa ratiba aliyonipangia huyu mtu asiyejulikana, itanilazimu nipoteze masaa zaidi ya 72 ya kazi kwa ajili ya kuhudhuria misa hiyo tu..."

"Usisahau kwamba muda wetu ni wa muhimu sana, hasa katika kipindi hiki ambacho matukio ya uhalifu yanajitokeza mfululizo."

Eddy aliongea kama anajitetea.

"Bosi, mimi naamini mtu aliyekutumia mali huu analijua hilo. Ndiyo maana akakutumia fedha za kutosha kufidia muda wako na pia kulipia gharama nyingine zinazoweza kujitokeza kwa sababu ya safari hiyo" Stella alisisitiza ingawa kwa sauti ya upole.

Maneno hayo yakamkumbusha Eddy zile dola zilizokuwa pale mezani. Akaziinua na kuziangalia tena kwa makini, kuhakikisha siyo fedha bandia.

Alipojiridhisha akaanza kuzihesabu kwa kutupia noti moja moja mezani. Zilikuwa jumla ya noti 55 sawa na dola 5,500 za Marekani. Akaziweka mezani, akamgeukia Stella.

"Najaribu kujiuliza huyu mtu ni nani? Ana jambo gani? Na kwa nini amenitumia fedha zote hizi?" Eddy aliuliza huku akimwangalia Stella machoni.

"Inawezekana ni rafiki yako wa zamani, ndugu, classmate, au mtu uliyewahi kumsaidia jambo fulani huko nyuma, lakini kwa sababu za ki-maisha mkapotezana..."

"Au pengine ni mpenzi wako wa zamani ndiyo maana hataki kujitambulisha ili mtakapoonana iwe furaha zaidi. Mambo ya suprise hayo!" Stella alijibu huku akimuangalia Eddy kwa macho ya wivu kidogo. Eddy akaangua kicheko.

"Hiyo inawezekana, na wala haitakuwa ajabu." Eddy alisema huku akiendelea kucheka. "Upo pia uwezekano kwamba mtu huyu ana taarifa nzito anayotaka kutupa au kututaka tui-chunguze..."

"Maana hiyo ndiyo kazi yetu hasa, lakini swali ninalojiuliza ni lilelile, kwa nini atangulize kutoa pesa nyingi namna hii? Anataka kuninunua au kuninyamazisha?"

"Kwanini unafikiria hivyo bosi?"

"Kwa sababu Mizani ina marafiki wengi, na maadui wengi pia. Kwa bahati mbaya marafiki zetu wengi ni watu wanyonge, wasiokuwa na uwezo mkubwa wa kifedha; lakini asilimia kubwa ya maadui zetu ni watu wakubwa serikalini na matajiri.

Watu ambao kiu yao ni kuhujumu uchumi wa nchi na kuivuruga serikali yetu tukufu ili mradi wapate maslahi binafsi."



Viaticum-4

Sakramenti ya Mwisho

Inatoka Uk. 28

“Hilo nalijua bosi”

“Ndiyo maana najiuliza mara mbilimbili, isije kuwa ni mtego wa kuniingiza kwenye kundi la wahalifu, au kujaribu kunibambikizia kesi ya rushwa.

Hebu fikiria watu wa taasisi ya kupambana na kuzuia rushwa wakituvamia ghafla muda huu, wakadai pesa hizi tumelipwa baada ya kumtishia kigogo fulani kwamba tuna stori yake tutamlipua gazetini! Si tutakuwa kwenye shida?”

“Mh! Bosi usemayo ni kweli, tumezungukwa na maadui kila upande. Tena nikikumbuka kifo cha inspekta Hatibu ndiyo huwa naishiwa nguvu kabisa...

Lakini pamoja na hilo najaribu kufikiria kwa upande mwingine, upendo wa huyo mtu. Kwa maana kama ni rafiki au mtu mliyepotezana kitambo kaamua kuku-suprize kwa kukutumia tiketi ya ndege na hizo dola ili uhudhurie hiyo misa muweze kuonana, halafu usiende, itakuwa mbaya sana. Utakuwa umemdhulumu furaha yake.”

“Uko sahihi Stella, maana hatuna namna ya kumrudishia fedha zake. Kama unavyoona hii bahasha haikuandikwa jina la mtu aliyetuma.

Sehemu ilipotakiwa kujazwa jina la mtumaji ameandika jina langu kinyume. Hii ina maana mtu huyo hakutaka ajulikane abadan, na pia ana hakika lazima nitaitikia wito wake”

“Sawa kabisa bosi. Tangu mwanzo hisia zangu zinanisukuma kuamini huyu ni mtu anakujuua vyema. Anajua wewe ni mtu unayeishi kwa kufuata kanuni na maadili.

Hivyo, si rahisi uchukue dola 5,500 kisha utokomee gizani. Ana uhakika wa asilimia tisini na tisa kuwa utaenda. Na hata kama usipoenda, basi yuko tayari kupoteza fedha zake bila kujuta. Kwa kifupi huyu si mtu wa kawaida”

“Kweli kabisa. Na hicho ndicho kitu kinachonifanya niamini kuwa huyu si rafiki wa

kwenda naye club au casino kucheza kamali.

Huyu ni muungwana mwenye taarifa nzi-to anayotaka tuifanyie kazi, au adui mwerevu anayetaka kuniingiza mtegoni. Yote mawili yanawezekana, ingawa sasa naanza kulipa uzito zaidi jambo la kwanza” Eddy alihitimisha.

“Kwa hiyo utakwenda?

“Hebu subiri kidogo” Eddy alijibu huku akinayanyua simu yake ya mkononi iliyokuwa juu ya meza. Akabonyeza namba kadhaa, kisha akaiweka sikioni kusikiliza wimbo uliokuwa ukichezwa upande wa pili wakati simu ikiita.

“Niambie bosi wangu,” sauti nyororo ya msichana iliita. Binti huyu alikuwa mfanyakazi wa shirika la ndege la Tanzania upande wa tiketi. Ofisi yake ilikuwa kwenye Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere.

Alikuwa mmoja wa watu muhimu na wa karibu sana na Mizani. Licha ya kusaidia kufanya booking za ndege pale zinapojitokeza safari za haraka, pia alikuwa mtoa habari muhimu.

“Habari za leo, Prisca?

“Poa tu mtu wangu, kwema?

“Kwema kabisa, mzee hajambo?

“Hajambo, niambie?

“Nataka ku-confirm kama kesho mna safari ya Mwanza”

“Tutakuwa na safari mbili, moja asubuhi na nyingine jioni, lakini ndege zote zimeshajaa?


“Nimekatiwa tiketi na mpenzi wangu mpya, unaweza kuangalia kama jina langu lipo kwenye orodha ya wasafiri?

“Nimeshaangalia, upo ndege ya jioni”

“Hapo ndipo unaponikosha. Uko sharp sana. Ahsante kwa msaada wako.”

Itaendelea wiki ijayo...





Onyo: Hakuna mafanikio kupitia miujiza ya dini

Inatoka Uk. 27

Mchungaji Hanaja:

Mchungaji mstaafu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania, Dayosisi ya Wazo, Dar es Salaam, Richard Hananja, anasema suala la kusa-ka miujiza linatokana na waumini wa siku hizi kutaka kuhubiriwa mambo mazuri tu na kua-cha ibada za kawaida za mahubiri ya kumjua na kumtii Mungu ili waende mbinguni.

Mchungaji Hananja ambaye kwa sasa ni Mkurugenzi wa Hananja Compassion Foundation anasema; “waumini wa siku hizi wanataka kusikia ibada za kufunguliwa, kila siku ni ibada za kufunguliwa, za kupokea gari, utasikia wana-ambiwa endesha gari, wanashikishwa simu wa-naambiwa wapige simu za kupata fedha, hawaji-ulizi nani anatoa hizo dola?” anasema.

Anaongeza; “hakuna tafsiri nyingine kwa hao watu, ni ushirikina tu wanafanya kwa jina la dini. Tukisema watu wanakasirika. Nadhani tu-waache wanaokwenda kwenye huo ujinga waba-ki na ujinga wao kwa sababu wale wanaowadan-ganya hawana kosa, watajuana na Mungu wao huko mbinguni. Ila hao wanaokwenda kwenye huo ujinga ndiyo wana makosa.”

Kanisa kiboko ya wachawi

Mfano wa hivi karibuni kuonyesha jinsi watu wanavyorubuniwa na hao wanaojiita manabii ni kutoka Kanisa la Christian Life Church lililoku-wa linaongozwa na Nabii Dominiki Dibwe, raia wa DRC.

Julai 25 mwaka huu - 2024, serikali kupitia kwa Msajili wa Jumuiya za Kiraia wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, alimwandikia barua Nabii Dibwe kutaka ajieleze kwa nini anatumia mahubiri yanayowadhalilisha watu.

Siku chache baadaye kanisa hilo lililokuwa Buza kwa Rulenge wilayani Temeke lilifungiwa na nabii huyo kurejeshwa kwao DRC.



Nabii Dominiki Dibwe

Sababu nyingine ya kufunguliwa kwa kani-sa hilo lililokuwa linaendeshwa na nabii huyo maarufu kama ‘Kiboko wa Wachawi’ ni kuwato-za fedha kiasi shilingi 500,000 waumini waliota-ka kuombewa, kinyume na kanuni za uendeshaji wa taasisi za kidini.

Aidha, mchungaji huyo anadaiwa kutoa ma-hubiri yanayohamasisha uchonganishi kwenye jamii ambapo anawahamasisha waumini kuua watu kwa imani za uchawi.

Ili kujiweka karibu na watawala, Januari, mwaka huu nabii huyo alitoa zawadi ya gari kwa Jeshi la Polisi kupitia Kituo cha Polisi Wilaya ya Chang’ombe, Dar es Salaam.

Dibwe alisema alitoa zawadi hiyo yenye tha-mani ya shilingi milioni 40 kwa jeshi hilo kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa shughuli mbalim-bali.

Hivi sasa nabii akiwa Kinshasa, DRC, ana-onekana katika vipande vya picha jongefu aki-wakejeli wale waliokuwa wanampatia shilingi 500,000 kwa ajili ya maombezi.


Anaonekana akijitapa kuwa anazitumia fed-ha alizokusanya kutoka kwa watu hao kuendesha maisha ya anasa na pia kujenga kanisa kubwa huko kwao ili kuendeleza huduma zake.

Na Hellen
NGOROMERA

Uhusiano



Kinachokera wanaume wengi kwenye uhusiano - 1



KARIBU msomaji wangu wa safu mahsusi inayohusu masuala ya uhusiano.

Wiki hii nitazungumza kuhusu matendo yanayowaudhi wanaume ambayo hufanyiwa na wake au wapenzi wao.

Ili familia istawi zaidi, inahitaji juhudi na nguvu kubwa kutoka kwa pande zote, mume (mwanaume) na mke (mwanamke). Kila mmoja ana majukumu yake ya kutekeleza.

Ingawa hivi sasa kuna mabadiliko sana, ambapo mgawanyo wa majukumu unaweza usiwe kama ule wa asili uliozoeleka.

Lakini cha msingi ni wawili hao kukubaliana jinsi ya kutekeleza majukumu hayo.

Hata katika mfumo wa sasa wa maisha, ambao mwanamke anaweza kuwa ndiye mtafutaji, lakini mwanaume anapaswa kubakia kuwa kichwa cha familia.

Kiasili, mwanaume anapaswa kuwa ndiye mwonyesha njia mkuu katika familia. Hii haimaani-shi kuwa mwanamke abweteke na kusubiri kuambiwa kila kitu na mwanaume.

Hata kama yeye si mtafutaji mkuu, mwanaume ana wajibu wa kuhakikisha familia inapata mahitaji yake yote ikiwemo chakula, mavazi, gharama za shule wka watoto, matibabu na burudani kwa kutaja machache.

Wanaume hutofautiana katika kupata kipato kwani wengine hutegemea mishahara kutokana na ajira zao na wengine hupata pesa kutokana na kazi zao (binafsi) kujiajiri na mambo mengine.

Katika pitapita zangu kikazi na kibinafsi niliweza kuzungumza na wanaume kadhaa kuhusu masuala ya uhusiano na wakanieleza machungu yanayowapata.

Mmoja alisema wanawake wengi wamekuwa wakiwatuhumu wanaume kwa mambo mengi yasiyo na mashiko hasa wanapochelewa kurudi nyumbani.

“Mara nyingi unaporudi nyumbani kwa kuchelewa maneno ya kwanza utakayokutana nayo kutoka kwa mwenzi wako ni ‘ulikuwa kwa mchepuko’, kauli hii huwa inatukwaza sana wanaume,” alisema mwanaume huyo.

Mwingine alisema wanawake pia huwazia mambo potofu kwa waume zao bila ya sababu za msingi.

“Mbali na kukuwazia ‘ujinga’ unapochelewa kurudi au unaposhindwa kufanya analotaka, pia wana tabia akikupigia simu ukachelewa kuipokea, unapoipokea tu hutoa maneno ya karaha! Wanawake wanaudhi sana.

“Wanasahau kwamba mwanaume huangaika kutafuta mkate wa familia ili kuifanya iendelee, muda wote hutuwazia mambo ya ajabu!

Wanaume huwa tunapambana kufa na kupona, lakini wake zetu wanasahau haya,” alisema mwanaume mwingine.

Maneno ya wanaume hao kiuhalisia kwa namna moja au nyingine, husababisha ndoa nyingi kuyumba na hata kuvunjika kabisa.

Pamoja na wanaume kuwa na udhaifu katika mambo kadhaa, lakini wengi wao hujali, hulinda na kuziwezesha familia zao kustawi.

Kwa mustakabali huo, wanawake wana wajibu wa kuwalinda na kuwalea waume zao kikamilifu na kuwapatika faraja hasa katika kipindi ambacho hupitia magumu katika kazi zao na kwa kufanya hivyo watawafanya kupata akili mpya na nguvu za kuendesha familia zao.

Inaumiza sana moyo pale ambapo mwanaume anapata shida kutafuta na unaporudi nyumbani au akipigiwa simu akutane na maneno yanayoonyesha kuwa alikuwa anahangaika na michepuko.

Kwa kiasi fulani, kwa baadhi ya watu, kauli kama hizi ndizo huwasukuma kweli kuanza kufuatilia michepuko kwa sababu wanajiona kuwa tayari wame-shahukumiwa kwa kosa ambalo hawajalifanya, kwa hiyo wanaona ni heri wafanye.

Tukutane wiki ijayo.

Kwa maoni na ushauri: hellen2ngoromera@gmail.com Au simu: 0754 88 67 49.

Mitindo & Urembo

Na Agatha Charles

Ficha tumbo
kwa kuvaa hivi

WANAWAKE wengi wanahangaika kwa kuwa na tumbo kubwa kutokana na sababu tofauti ikiwemo kujifungua watoto.

Kutokana na hilo, wengi hushindwa kuvaa baadhi ya nguo kwa kuhofia tumbo kuonekana kubwa huku wapo pia wasiojali hilo.

Kupitia safu hii, nimekuwekea baadhi ya aina za nguo ambazo zitakusaidia kukupa ujasi-ri wa kuvaa na kwenda kokote unakotaka.

*Peplum; hii inaweka kuwa blauzi au gauni ambayo ina muundo wa kufunika tumbo.

Unaweza kushona au kununua inayofunika kote hadi nyuma ama ikafunika mbele tu eneo la tumbo.

*Vaa gauni pana kisha funga mkanda kwa juu. Hii inasaidia kwa kuwa mkanda unafunga juu ya tumbo hivyo inapunguza muonekano wa ukubwa wa tumbo lako.

*Vaa nguo zenye mistari iliyosimama, epuka kuvaa zenye mistari iliyolala kwani zitakufanya mnene zaidi na tumbo kuchomoza.

*Vaa nguo nyeusi, iwe gauni au blauzi itakubeba na kukufifisha tumbo au kama una umbo pana utaonekana umepungua kidogo.

Nywele
zimekatika?

*Tumia kitunguu maji, tangawizi NYWELE zinaweza kukatika kutokana na mambo mengi, ikiwemo namna unavyozitunza, kusuka ama maradhi.

Ipo tiba ambayo haitumii gharama kubwa na yenye matokeo ya haraka kwa kutumia tangawizi na kitunguu maji.

*Tangawizi imeshehe-ni madini ya Magnesium Potassium, Phosphate pamoja na vitamini ambavyo kwa pamoja hufanya kazi ya kupipa nywele afya na hivyo kuzuia kukatika kwa urahisi.

*Kitunguu maji kinasaidia kupambana na bakteria wanaoweza kusababisha magonjwa ya ngozi ya kichwa kama mba ambao huchangia kukatika kwa nywele.

Jinsi ya kutengeneza

*Saga mchanganyiko wa tangawizi na kitunguu maji baada ya kukiosha, kisha chuja na paka mchanganyiko huu kwenye ngozi ya kichwa chako.

*Funika kichwa kwa kofia ya plastiki kwa muda wa dakika 15 na baada ya hapo osha nywele zako kwa shampoo na maji ya baridi.

* Fanya hivyo angalau kila wiki kwa matokeo mazuri zaidi.

Afcon



Iko wapi timu yetu ya Afcon 27?

Na Mwandishi WETU

WIKI iliyopita viongozi kadhaa wa soka Afrika, walitembelea na kukagua kazi ya ujenzi wa viwanja vya michezo vitakavyotumika katika fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon 2027) ambapo Tanzania itashirikiana na Kenya na Uganda kuandaa.

Viwanja hivyo vinajengwa katika maeneo mbalimbali nchini chini ya juhudi za serikali kupitia Wizara ya Michezo, Sanaa na Utamaduni.

Ni dhahiri kuwa juhudi hizi zinazoendelea za maandalizi ya miundombinu kwa ajili ya michezo hiyo zitafikia malengo yake ya kuifanya nchi kuwa na miundombinu bora kama ambavyo wamiliki wa mashindano hayo, Shirikisho la Soka Barani Afrika – CAF, wanavyotaka.

Lakini, ushiriki wa Tanzania katika mashindano hayo unakwenda mbali zaidi ya kuandaa miundombinu bora, kwani itakuwa ni moja ya nchi zitakazoshiriki mashindano hayo kupitia timu yake, Taifa Stars.

Ni ndoto ya kila mpenda michezo nchini kuona timu hiyo ya Tanzania ikifanya vizuri katika fainali hizo na pengine kuweka historia ya kunyakua kombe hilo.

Lakini mafanikio hayo hayatakuja kama muujiza, yanatakiwa maandalizi kabambe kujenga timu imara itakayoweza kushindana na kupata ushindi.

Ajabu ni kuwa tunafanya maandalizi ya miundombinu ambayo kwa kweli yanaonekana kwenenda vyema, lakini bado mpaka hivi sasa umma haujaambiwa mipango ya kuandaa timu kabambe itakayotoa ushindani wa nguvu kwenye fainali hizo.

Kama kuna anayedhani Taifa Stars itafan-

ya vizuri kwenye Afcon 2027 kwa sababu tu nchi imeandaa viwanja vizuri na miundombinu mingine, basi aamshwe, maana anaota ndoto.

Hivi karibuni Tanzania imeshuhudiwa iki-abulia patupu kwenye Michezo ya Olimpiki huko Ufaransa, na hii imesababishwa na kuwepo maandalizi hafifu.

Siyo ajabu kwamba Tanzania inasubiri hadi 2026 ndio ikurupuke na kuanza kuandaa timu. Na Taifa Stars ikishindwa mwaka 2027, nchi itarudi tena kushauriana kuhusu umuhimu wa maandalizi!

Hivi karibuni kuliibuka mjadala mkubwa kuhusu kaimu kocha mkuu wa Taifa Stars, Hemed Morocco alipotangaza wachezaji wa Timu ya Taifa na kuwaacha Mbwana Samatta na Simon Msuva.

Mijadala ilikuwa mingi watu wakihoji kwa nini mashujaa hao wa taifa wameachwa kwenye timu hiyo, wengi wakiamini kuwa bado tunapaswa kuendelea kuwategemea wachezaji hawa.

Ni kweli kuwa Samatta na Msuva wametufanyia mambo makubwa, lakini ni dhahiri pia kuwa wakati wao unafika mwisho.

Kama Tanzania ingekuwa na maono na mtazamo mpana wa maendeleo ya soka, basi ingekuwa imeshaandaa warithi wao mapema kwa sababu hawa siyo wa kuwategemea kutubeba kwenye Afcon 2027.

Watu wengi wanaona Taifa Stars ikishindwa mapema kwenye fainali hizo kwa sababu kama nchi ingekuwa na dhamira ya kufanya vizuri, ni dhahiri kuwa hivi sasa ingekuwa kwenye utekelezaji wa programu ya kuandaa timu itakayoshiriki fainali hizo.

Lakini hadi hivi sasa hakuna kinachosikika kuwepo kwa mipango ya kuandaa programu hiyo. Na kama ipo, kimya ni wa nini?



Jux kufunga ndoa na mrembo wa Nigeria

Lagos, NIGERIA

MSANII wa bongo fleva, JUX anatarajia kufunga ndoa na mrembo kutoka Nigeria, Priscy.

Tayari nyota huyo wa bongofleva ameshafanya taratibu za kwenda kujitambulisha ukweni nchini Nigeria na kupokelewa na familia ya mwanamke huyo.

Jux miezi michache iliyopita alimtambulisha mpenzi wake huyo mwenye asili ya Nigeria kupitia mitandao ya kijamii na wanazengwe wakisema kuwa haya yana muda, wakimaanisha hataka milisha taratibu za ndoa.

Jana ikiwa siku ya kuzaliwa ya Msanii huyo, mpen-

zi wake amemtakia heri ya kuzaliwa kupitia posti yake ya Instagram kwa kandika 'Heri ya kuzaliwa kwa Mpenzi wa Maisha Yangu JJ wangu! Umenionyesha maana halisi ya upendo wa kweli na umeleta furaha kubwa maihani mwangu milele. Wewe ni mtu wa ajabu sana, na natamani dunia ingejua jinsi moyo wako ulivyo mkubwa.

Aliendelea kwa kuandika "Unanifanya nihisi kama msichana mdogo kila wakati, na ninaomba siku hii Mungu aendeleo kukubariki, kuongoza, na kukulinda kwa ajili yangu. Asante kwa kuni-penda na kuniruhusu niku-pende. Nakupenda sanaaaaa mpenzi, wewe ndiye ufunguo wa moyo wangu milele"

Wakazi 'awachana' Rosa Ree, Rayvanny

Dar es Salaam, TANZANIA

MSANII wa Rap na Bongo fleva Webirro Wassira maarufu kama Wakazi amewatolea uvivu wasanii wenzake Rayvanny pamoja na Rosa Ree wiki hii kwa kuponda tuzo za muziki wa bongo fleva.

Webiro aliwachana kwa kuandika, "Kuwa na Tuzo zenye mapungufu ni bora kuliko kutokuwa na Tuzo kabisa!! Maana zikiwepo, as flawed as they might be, hiyo ni dalili ya kuwa tunaelekea in the right direction.

Alimalizia, Rayvanny ni mwana, ila sijapenda alichofanya! kumbuka kuwa nominated tu ni ushindi tosha.

TG Omori awashukuru mashabiki zake

Lagos, NIGERIA

MUONGOZAJI wa Video kutoka nchini Nigeria, ThankGod Omori Jesam anayejulikana kama TG Omori amewashukuru mashabiki wake kwa msaada wao wa kiroho na kisaikolojia.

Omori ambaye alikuwa akisumbuliwa na maradhi ya figo yaliyosabisha kufanyiwa upasuaji wa upandikizaji wa figo wiki chache zilizopita na sasa anaendelea vizuri.

TG kupitia mtandao wake wa X ameandika "Asanteni nyote kwa maombi, naendelea kupona mshono wa upasuaji, Nitaendelea kupambana, nimekuwa kwenye vita hii kwa zaidi ya mwaka mmoja au miwili na siwezi kurudi nyuma sasa. Nawapenda sana. Siwezi kusubiri kutengeneza video mpya za muziki za watu wengi kwa ajili yenu".



Na John MARWA

MNYAMA na mishe zake, watu na maono yao, ndivyo unaweza kueleza kutokana na kile ambacho kikosi cha wekundu wa Msimbazi, Simba wanakionyesha msimu huu mpaka sasa.

Licha ya upya wa kikosi chao na benchi la ufundi chini ya Kocha Fadlu Davis, kuna maiisha ambayo Mnyama Simba ameanza kuyaishi tofauti na mtarajio ya wengi.

Hii ni baada ya kuonyesha makali kwenye ligi ambapo Mnyama kachukua pointi zake sita na mabao saba katika michezo miwili akiwa kileleni mwa Ligi ya NBC.

Pia ameonyesha cheche mwishoni mwa wiki katika mchezo wa kirafiki wa kimataifa dhidi ya Al Hilal ya Sudan katika Dimba la KMC Complex na kutoka sare ya bao (1-1).

Katika mchezo huo, Simba walionyesha ustadi mkubwa wa kumiliki mchezo na kuweka shinikizo kwenye kila tukio jambo ambalo liliwafanya Al Hilal, licha ya kukaa katika eneo lao muda mwingi, kuweza kuruhusu bao kwa kulazimishwa kufanya makosa na Simba kuyatumia kupitia kwa mshambuliaji wao mpya, Lionel Ateba.

Kipindi cha pili kilikuwa na picha mbili tofauti; kwa makocha wote wawili, Kocha Fadlu na Kocha Florent Ibenge, ambapo Fadlu alitaka picha ya kila mchezaji katika mechi kubwa,

huku Ibenge akiongeza gia ya kulazimisha Simba kufanya makosa na kila mmoja akafaidika kivyake. Kiwango cha Simba kimekuwa kikiwafanya wadau wa soka baadhi kuhisi timu yao bado ni ya kawaida na wengine wanaamini iko kwenye kujipanga zaidi kwa mafanikio makubwa msimu huu.

Ni wazi kwa jicho pevu Mnyama ana mishe zake na watu wana maono yao. Kuna njaa inaonekana kuanzia kwa wachezaji wapya na waliokuwepo, benchi la ufundi, uongozi hadi mashabiki.

Ukiwatazama Simba katika maeneo mataatu uwanjani; eneo la ulinzi wameimarika sana, eneo la kiungo wameboreka sana na eneo la ushambuliaji, wanapambana.

Ni Simba ambayo inaonyesha kuhitaji kiti chake, ni Simba ambayo itawashangaza wengi, lakini haiondoi ukweli kwamba ndio kwanza wako gia namba moja.

Wiki mbili zijazo Simba ataanza mishe zake kwenye Kombe la Shirikisho dhidi ya Al Ahly Tripoli ya Libya katika mchezo wa mkondo wa kwanza kabla ya kurejeana Uwanja wa Benjamin Mkapa na mshindi wa jumla kutinga makundi.

Ni michezo ambayo Simba atahitaji kuonyesha mishe zake msimu huu na walio na maswali na kigugumizi kuungana na mishe zake msimu huu ama kuendelea na maono yao.

MICHEZO

Jumatatu, Septemba 2-8, 2024



Stars na tumaini jipya Afcon 2025

Na John MARWA

NI takribani miezi saba tangu Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon 2023) zilizofika tamati kwa wenyeji Ivory Coast kutwaa ubingwa wa tatu katika historia yao.

Safari ya kuzisaka timu 24 katika michuano inayofuata inaanza rasmi wiki hii.

Timu ya Taifa ya Tanzania, 'Taifa Stars' ambayo ilishiriki kwa mara ya tatu - baada ya kufanya hivyo 1980, 2019 na 2023 na sasa iko 'kamili gado' kuisaka Afcon ya nne kabla ya kuwa mwenyeji katika michuano ya 2027.

Kikosi cha Stars kiko kambini kujiwinda na wapinzani wao Ethiopia, ambapo mtanange utakaopigwa kesho kutwa, Jumatano hii katika Dimba la Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, kusakana nafasi ya kuelekea nchini Morocco ambao watakuwa wenyeji.

Licha ya kikosi cha Taifa Stars kuwa na mseto

wa vijana, lakini bado matumaini ni makubwa kwa Kocha Hemed Morocco ambaye anajukumu zito la kuipeleka tena Tanzania Afcon 2025 kama sehemu ya maandalizi ya kuwa wenyeji 2027.

Morocco ameonyesha imani kubwa kwa vijana huku akimiani kuwa ni wakati wao kufanya vizuri na kulitumikia taifa kwani muda ni sasa.

Takwimu zinaonyesha Stars kuwa nyuma ya Ethiopia, kwani katika michezo mitano ya mwisho yalipokutana mataifa hayo, Ethiopia ilishinda mara mbili huku sare ama suluhu zikitoika mara tatu.

Baada ya mchezo huo wa September 4, Stars itakuwa na kibarua kingine dhidi ya Guinea, September 11 huku mpinzani mwingine katika kundi hilo, ni DR Congo.

Ni timu mbili pekee zitakazojikusanyia pointi zaidi katika kila kundi kufuzu Afcon 2025, ambapo Tanzania, Ethiopia Guinea na DR Congo zitamenyana haswa.

GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa mzunguko - kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.

